SUPA JACKPOT
TZS. 1,096,041,286
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mbaroni** madai mauaji, kunyofoa sehemu za siri

UKURASA 3


siasa
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe
JUMATANO MACHI 29, 2023
Aambiwa ni mtizamo wa ki-AZAKI si wa wanasiasa wanaotamani dola
Juhudi ushirikiano mpya kimkakati kuzuia kasi, ushawishi China, Urusi
KARIBU KAMALA HARRIS DAR
**Tanzania na Afrika zitapaa kiuchumi iwapo Amerika itawekeza kwenye nishati**

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Machi 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581264


www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

# 'Adhabu kifo ifutwe'

UKURASA 3





Nyumba ikiwa imebomoka upande katika eneo la Msimbazi Magharibi, Tabata jijini Dar es Salaam kutokana na mvua iliyonyesha jana. **Picha ndogo:** Mmoja wa wapangaji wa nyumba hiyo, Kondo Musa, akiokolewa na wasamaria wema baada ya kunusurika kifo. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Mvua yajeruhi, yabomoa nyumba, barabara

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WALALAMIKIA MFUMO MALIPO KIELEKTRONIKI KUDHULUMU CHENJI**

WATUMIAJI wa vivuko vya Kigamboni mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia mfumo wa kadi za kielektroniki unaotumika kwenye malipo ya kivuko...

UKURASA WA 4

**LHRC YALIA NA SHERIA NDOA YA MWAKA 1971**



KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimeibua hoja sita zinazopinga Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kwa...

UKURASA WA 5

**ZAIDI YA WALIMU 10,000 WAJENGEWA UWEZO**

MRADI bunifu wa elimu wa Shule Bora umefanikisha kuwajengea uwezo walimu zaidi ya 10,000 kwa kuwapa mafunzo kuboresha ufundishaji na...

# Odinga alaani uvamizi mali za Kenyatta

UKURASA 19



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga na Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki, wakionyesha vipande 25 vya meno ya tembo vilivyokamatwa jijini Mbeya juzi. **Habari Uk. 16. PICHA: NEBART MSOKWA**

**MICHEZO** **KAKOLANYA AITESA SIMBA SC** UK.24 **KATUNI** UK.6



Shekhe Mkuu wa Tanzania, Mufti Dk. Abubakar Zubeir Bin Ally (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kushoto), wakikabidhi msaada wa futari kwa kituo cha kulelea watoto yatima cha Safina, Tuangoma jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na Benki ya CRDB. Wengine ni Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Wallid Alhad Omar (wa pili kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (wa nne kushoto) na viongozi wengine wa BAKWATA na viongozi wa kituo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mvua yajeruhi, yabomoa nyumba

**Waandishi Wetu**

MVUA za masika zinazoendelea kunyesha maeneo tofauti nchini, zimesababisha athari katika mikoa mbalimbali ikiwamo kujeruhi, nyumba kadhaa kubomoka na baadhi ya barabara kukata mawasiliano.

Katika tukio lililotokea jana, Msimbazi Magharibi, Tabata jijini Dar es Salaam, mkazi wa eneo hilo, Kondo Musa (28), amenusurika kifo baada ya kuangukiwa na ukuta wa nyumba aliyokuwa anaishi na wapangaji wenzake wanne.

Akizungumza na Nipashe, majeruhi huyo alisema alirudi nyumbani kwake jana asubuhi kwa ajili ya kubadilisha nguo ndipo muda mfupi baadaye mvua ikanyesha akiwa amelala.

"Nikiwa nimelala, nilishtuka baada ya kusikia kishindo na ukuta umenijeruhi maeneo ya tumboni na miguuni," alisema.

Mjumbe wa Shina Namba 11, Nungano Kivuruge, alisema nyumba iliyoanguka ilikuwa na ufa wa muda mrefu.

"Tukio hilo limetokea kwenye eneo langu. Nyumba ina vyumba vinne, mwenye nyumba anafahamika kwa jina moja Mhagama," alisema.

Mjumbe wa Mtaa Msimbazi Magharibi, Beth Joel, alisema: "Nikiwa ofisini alikuja mjumbe kutoa taarifa ya kuanguka kwa nyumba hii kutokana na mvua iliyonyesha leo (jana)."

Alisema ndani ya nyumba hiyo, kulikuwa na wapangaji wengine watano ambao wao walifanikiwa kukimbia baada ya kusikia kishindo cha kuanguka kwa ukuta huo. Alisema viongozi wa mtaa wamekubaliana kukutana na kukagua nyumba zote ambazo zina nyufa ili kuwashauri wakazi wake wasilale humo.

Fatuma Said, mmoja wa wapangaji wa nyumba hiyo, alisema wakati akiendelea kupika chumbani kwake, alisikia kishindo cha ukuta ukianguka.

"Nilipotoka nje nikakuta ukuta wa chumba cha nje umeanguka na huyu kaka alikuwa amelala ndipo wapangaji wakakimbilia nje," alisema.

Wakati hayo yakitokea Dar es Salaam, huko Tarafa ya Mukulat iliyoko Arumeru mkoani Arusha, mvua zilizonyesha juzi zimebomoa makazi na nyumba zingine kujaa maji na wananchi wake kukosa mahali pa kukaa.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, alisema jana kuwa kutokana na tishio la mvua hizo, Jeshi la Polisi limemwarifu kwamba mpaka sasa hakuna mtu aliyepoteza maisha.

"Kumekuwa na uvumi uliosababisha taharuki kwa baadhi ya wananchi kwamba mvua hizi zimesababisha vifo vya watu watatu waliokuwa wamepanda pikipiki moja baada ya chombo hicho kukutwa kikiwa kimefunikwa kwenye kifusi cha tope katika eneo la Kibaoni, Ngaramtoni," alisema.

Alisema uchunguzi uliofanywa na polisi, umeonyesha hakuna mtu aliyepoteza maisha na mmiliki wa pikipiki hiyo amethibitisha kwamba watu hao walijiokoa.

"Jeshi la Polisi lilifanya uchunguzi wa kina ikiwa ni pamoja na kumtafuta mmiliki halali wa pikipiki hii na alithibitisha kuwa watu hawa ambao ni wanaume wawili walifanikiwa kujiokoa wenyewe na watatu ambaye ni mwanamke aliokolewa na wasamaria wema, usiku wa Machi 23, mwaka huu," alisema.

Alisema kulingana na tathmini iliyofanywa na wataalamu waliotembelea maeneo yaliyoathirika na mafuriko, uwapo wa uchafuzi wa mazingira, hasa utupaji wa taka ngumu ambazo zimesababisha mitaro kuziba na kushindwa kupitisha maji.

Mvua hizo zimesababisha uharibifu wa mali za wananchi katika Kata za Oltrumet, Oloirien, Sambasha, Olmotonyi na Kimnyaki, ingawa serikali haijaweka hadharani taarifa ya idadi ya makazi yaliyoharibiwa.

Mkoani Iringa, mvua zilizonyesha juzi kwa zaidi ya saa nne katika mji wa Iringa, zimesababisha athari ya miundombinu eneo la Mkimbizi Bima na baadhi ya maeneo ya Manispaa ya Iringa baada ya barabara inayounganisha kata hiyo na Mtwivila kuwa hatarini kukatika.

Wakazi wa eneo hilo, Silla Kimwanga na Sara Sanga walisema mvua hizo zimesababisha sehemu kubwa ya barabara kukatika.

Kimwamga alisema eneo ambalo barabara hiyo inakaribia kukatika awali Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Manispaa ya Iringa, walijenga mtaro kwa kuweka karavati.

Alisema eneo hilo kuna karavati ambalo limeziba halipitishi maji hivyo kusababisha kupita juu ya barabara na kuleta madhara makubwa maeneo hayo.

"Kero hii ni kubwa kwetu na barabara hii inaunganisha Kata ya Mtwivila na endapo haitafanyiwa kazi mvua zikiendelea upo uwekezano wa watumiaji wake kukosa mawasiliano," alisema.

Diwani wa Mkimbizi, Eliud Mvella, alisema eneo hilo linahitaji ufumbuzi kwa kuwa ni moja ya barabara muhimu.

Naibu Meya wa Manispaa ya Iringa, Juli Sawani, alisema sehemu kubwa ya manispaa imekumbwa na madhara na tathmini inafanywa na madiwani wa kata husika.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Iringa, Barnaba Jabiry, akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, alikiri kuwapo kwa madhara ambayo TARURA imeyapata kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha huku akisema baadhi ya barabara zimefungwa kutokana na kukatika.

***Imeandaliwa na Shufaa Lyimo (DAR), Allan Isack (ARUMERU) na Francis Godwin (IRINGA)***

# Kigamboni walalamikia mfumo kielektroniki kudhulumu chenji

**Na Christina Mwakangale**

WATUMIAJI wa vivuko vya Kigamboni mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia mfumo wa kadi za kielektroniki unaotumika kwenye malipo ya kivuko kuwadhulumu chenji zao.

Uchunguzi wa Nipashe uliofanyika ndani ya wiki moja, umebaini kuwapo kwa hali hiyo ambayo hata hivyo, mamlaka husika ilipoulizwa imesema tayari imeshatatua tatizo hilo.

Kilichobainika kuwa watumiaji wa vivuko wanapotoa malipo ya huduma hawarudishiwi chenji zinazobaki kwenye kadi zao huku watoa huduma wakilalamikiwa kutotoa ushirikiano wanapowasilishiwa madai.

**Huwa naweka fedha haizidi Sh. 1,000 au 2,000, na nauli ni Sh. 200 kwa safari moja lakini, ajabu kiwango cha kuweka kinaanzia Sh. 500, nikienda inakatwa Sh. 200 na kurudi Sh. 200 cha kushangaza Sh. 100 huikuti, tunahoji zinakwenda wapi?**

Fausta John, aliliambia gazeti hili kwamba, kuna changamoto katika matumizi ya kadi za mahali hapo.

"Unaweza kuweka salio la Sh. 1,000 wakati unavuka, ukirudi ukiweka kadi inakataa, inaonyesha salio hakuna. Kwa sasa nimeacha kutumia kadi zao, nakwenda na Sh. 200 yangu, nampatia mwenye kadi anichanjie," alisema.

Denis Baraka alisema; "huduma sio shirikishi, unafyekwa salio kimya kimya. Matumizi ya kadi kwenye vivuko ni mazuri, lakini yamekuja na changamoto ya kuchukua fedha za wananchi kielektroniki.

Mkazi wa Kinondoni, Maria Shampawe ambaye hufanya shughuli zake Kigamboni, alisema mfumo ulipoanza kila mtumiaji alipaswa kununua kadi kwa Sh. 1,000 na kutakiwa kuijaza kulingana matumizi yake.

"Huwa naweka fedha haizidi Sh. 1,000 au 2,000, na nauli ni Sh. 200 kwa safari moja lakini, ajabu kiwango cha kuweka kinaanzia Sh. 500, nikienda inakatwa Sh. 200 na kurudi Sh. 200 cha kushangaza Sh. 100 huikuti, tunahoji zinakwenda wapi?"

Mkazi wa Kigamboni Musa Haji alisema; "hili tatizo linaweza kufyeka salio hata mara mbili, tatu au kukomba salio lote na mteja asielewe salio lake limekatwaje."

Mkuu wa Kivuko cha Magogoni, Abdulrahman Ameir, kilicho chini ya Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), alisema tatizo hilo lilikuwapo kwa baadhi ya watumiaji wapya kutokana na kutofahamu namna ya kuchanja kadi zao.

"Inatakiwa kabla hujachanja kadi yako, unarudi nyuma hatua moja, ndipo uchanje ili geti lifunguke na kwenda wengine hawajui. Huwa tunatangaza kwa kuelewesha. Hilo tatizo limetatuliwa na lilikuwapo na kama linaendelea tunatoa elimu kila mara ya kuwaelimisha wateja.

Alisema changamoto zinazojitokeza kwenye mfumo wa kulipia nauli ya kivuko uitwao 'N-card', unaotumiwa na Kivukoni Kigamboni, zinatokana na uelewa duni miongoni mwa abiria ambao wengi wao ni wageni wa mfumo huo.

Ameir alisema elimu imekuwa ni endelevu kutokana na kubaini tatizo hilo, tangu mabadiliko ya ulipiaji kwa mfumo huo ulioanza mwishoni mwa mwaka jana kwa lengo la kuboresha huduma kielektroniki.

## Watu sita mbaroni kwa tuhuma za mauaji, kunyofoa sehemu za siri

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU sita wamekamatwa na polisi wakituhumiwa kujihusisha na vitendo vya mauaji, kufukua makaburi wilayani Manyoni na kuchukua sehemu za siri za miili ya watu waliozikwa kwa ajili ya kutengeneza dawa ya kupata utajiri na kuwauzia wateja wao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Stella Mutabihirwa, katika taarifa yake jana kwa vyombo habari, alisema watuhumiwa hao ambao hakuwataja majina kwa kuwa uchunguzi bado unaendelea, walikamatwa kutokana na msako uliofanywa na jeshi hilo kuanzia Machi 16 hadi 24, mwaka huu katika maeneo mbalimbali wilayani Manyoni na vijiji jirani vya Wilaya ya Sikonge, mkoani Tabora.

Alisema watuhumiwa hao baada ya kukamatwa na kuhojiwa walikiri kuhusika na mauaji ya mtu mmoja mwanamume ambaye hajafahamika jina mwenye umri kati ya miaka 40 na 45 yaliyotokea Machi 3, mwaka huu eneo la Relini Manyoni huku kifo chake ikisadikiwa kilitokana na kukanyagwa na treni kichwani na mguu wa kushoto.

Kamanda Mutabihirwa alisema baadhi ya viungo vya mtu huyo vilikuwa pembeni ya kiwiliwili katika njia ya treni huku viungo vya sehemu za siri vikiwa vimenyofolewa.

"Tulivyowahoji watuhumiwa walikiri kuhusika na tukio hilo na kueleza kwamba walikata sehemu za siri kama nywele, kucha na ulimi kwa lengo la kutengeneza dawa ili kuwapatia wateja wao wanaohitaji utajiri," alisema.

Aliongeza kuwa watuhumiwa hao pia wamekiri kujihusisha na vitendo vya kufukua makaburi wilayani Manyoni na kuua watu kwa lengo la kupata sehemu za viungo vya binadamu kwa ajili ya kutengeneza dawa ya kupata utajiri.

"Katika kukamilisha upelelezi wetu Jeshi la Polisi lilifanya upekuzi katika nyumba ya mtuhumiwa mmoja wao na kufanikiwa kukuta suruali moja nyeusi ya marehemu aliyeuawa Machi 3, 2023, vibuyu viwili vyenye shanga, kibuyu kimoja chenye ngozi ya kondoo," alisema.

Kamanda Mutabihirwa alisema vitu vingine vilivyokamatwa kwa mtuhumiwa huyo ni pembe ya kondoo yenye kioo na shanga, pembe ya ng'ombe yenye vipembe viwili vidogo, vipande vitatu vya sanda, kaniki vipande viwili, kitambaa kimoja chekundu na kopo la mafuta yenye mchanga wa kaburi na nywele.

Kutokana na hali hiyo, Polisi imetoa wito kwa wananchi kuachana na imani potofu za kishirikina na badala yake wafanye kazi kwa bidii kupata utajiri halali.



Meneja Msaidizi wa BRAC tawi la Ipagala, Cecilia Mwaikambo, akitoa mafunzo ya elimu ya fedha kwa wanafunzi zaidi ya 300 wa Shule ya Sekondari Makole, jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Fedha Duniani yanayofanyika kila mwaka mwezi Machi, yenye lengo la kuhamasisha utoaji elimu ya fedha kwa watoto na vijana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Pinda apendekeza adhabu ya kifo ifutwe

**Na Restuta James**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amependekeza marekebisho ya sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 kifungu cha 197, ili adhabu ya kifo ifutwe na badala yake, mshtakiwa anayekutwa na hatia ya mauaji au uhaini, afungwe maisha gerezani na kuitaka Tume itafute maoni zaidi.

Aidha, Pinda ameshauri mfumo wa hakijinai uweke utaratibu wa kulelewa kwa mtoto anayezaliwa na mfungwa anayetumikia kifungo gerezani.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa maoni yake mbele ya Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Haki Jinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu, Othman Mohamed Chande.

"Adhabu ya kunyonga mtu, inanipa tabu kwa sababu ni kweli alitoa roho ya mtu...na yeye tumnyonge? Kosa juu ya kosa. Sidhani kama inatibu (adhabu ya kunyonga), ugonjwa huo," alisema.

Pinda alisema adhabu ya kunyongwa hadi kufa haina tija kwa sababu mkosaji hapati nafasi ya kujirekebisha, akieleza kifungo cha maisha kitatoa nafasi ya mfungwa kujifunza na kujutia makosa yake.

"Kubwa kwangu ni ile principle (kanuni) tu, kwamba unaua na wewe unauawa. Nimewaambia waliangalie tuone, nchi nyingi zilishaondoa vitu hivyo," alisema.

Kuhusu mtoto anayezaliwa gerezani, Pinda alisema: "Mama anapokumbwa na janga la mauaji na huku ni mjamzito, anapelekwa rumande, anajifungulia huko, shida yangu ikawa ni kwamba mtoto huyu tusimwache katika eneo hili la magereza."

Pinda alisema mazingira yatamwathiri mtoto huyo kisaikolojia na kupendekeza waunganishwe na vituo vinavyolea watoto.

"Na hili nimelisema kwa sababu mazingira ya magereza ni magereza tu."

Alisema wanawake wanaojifungua wakiwa magereza hawapati mazingira mahsusi ya kuwawezesha kulea watoto ikiwamo vyakula vinavyoweza kuongeza maziwa.

Aidha, aliishauri tume kukusanya maoni kutoka kwa makundi yote wakiwamo madereva wa bodaboda, daladala, malori na mabasi; pamoja na makundi yenye malalamiko kwa Polisi, Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), zimamoto na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP), ili iweze kutoa ushauri utakaoleta tija kwa nchi.

Alipendekeza kuwa mnyororo wa hakijinai unapaswa kuangaliwa kuanzia Polisi, TAKUKURU, DPP, Mahakama na Magereza, ili wananchi wasiumizwe katika hatua yoyote ya kutafuta haki.

Alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuunda tume hiyo akieleza kuwa kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi kuhusu mifumo ya hakijinai.

"Malalamiko ni mengi, kila unapozunguka unakutana na watu wanalalamika. Pamoja na kukutana na makundi ambayo wamekwishayaainisha, lakini wajaribu kuangalia kila chombo eneo la malalamiko halafu tuone kama tunaweza kukutana na wadau kwenye hilo eneo," alisema.

Alitoa mfano wa malalamiko ya rushwa kwa askari wa barabarani pamoja na wapelelezi, Tume iwaite madereva wa vyombo vya moto ili wajue tatizo lililopo.

Kuhusu magereza, alisema eneo la kurekebisha tabia kwa wafungwa lipewe uzito ili wanapokuwa gerezani watoke na ujuzi.

Alisema shirika la uzalishajimali la Magereza lizalishe bidhaa zake kwa kutumia wafungwa na uwepo mfumo wa kuwafuatilia wanaotoka gerezani wakiwa na ujuzi ili kupima mafanikio ya marekebisho ya tabia ya mhusika.

#### WEREMA ATAKA MLUNDIKANO WA KESI UONDOLEWE

Mwanasheria Mkuu wa Serikali mstaafu, Jaji Frederick Werema, amewashauri majaji na mahakimu kumaliza msongamano wa kesi mahakamani kwa kufuta kesi zisizo na ushahidi wa kutosha.

Alisema mwaka 1996, aliwahi kuachia watuhumiwa 50 wa makosa ya jinai kwa siku moja, baada ya kupitia mafaili ya kesi zao na kubaini kwamba hakukuwa na ushahidi unaoweza kuwatia hatiani.

Kuhusu dhamana, alipendekeza marekebisho yafanyike ili mahakama iwe na mamlaka ya kutoa au kunyima dhamana badala ya inavyofanyika sasa kwa DPP kuwa na nguvu ya kuzuia haki hiyo.

Kadhalika, alipendekeza sheria ya utakatishaji fedha irekebishwe ili kupunguza makosa kutoka 28 yaliyopo sasa hadi manne, kwa kuwa ilivyo sasa inatumiwa vibaya na baadhi ya maofisa wa DPP 'kuwapa' watu kesi zisizo na dhamana.

Akizungumzia adhabu ya kunyonga, Jaji Werema alisema sio adhabu stahiki kwa kuwa haipi mfungwa nafasi ya kujifunza.

Alisema asilimia kubwa ya wanaofanya mauaji ni watu wenye kipato cha chini akitoa mfano wa mauaji yanayotokana na wivu wa mapenzi na ugomvi kwenye vilabu vya pombe za kienyeji.

"Adhabu inafundisha, sasa ukinyongwa umefundishwa nini? Adhabu ya kunyonga ibaki kwenye sheria kama tishio kwa sababu inaweza kutokea ikabidi unyonge maana kuna watu wanafanya mauaji ya kishenzi," alisema.

Kuhusu sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, Jaji Werema alisema amewasilisho marekebisho mengi ambayo hata hivyo, hakuyataja.

Akizungumzia kesi za jinai, ametaka zipewe nafasi kusikilizwa kama inavyofanyika kwenye kesi za madai.

#### MAGAI ALIA NA DPP

Wakili mwandamizi Sadock Magai, amependekeza DPP apunguziwe madaraka hasa yanayomruhusu kuzuia dhamana.

Alitaka marekebisho kwenye kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), ili kazi hiyo iachiwe mahakama.

Wakili Magai kutoka kampuni ya uwakili ya IMMMA, alisema kifungu hicho kimekuwa 'kichaka' cha baadhi ya maofisa wa DPP wasio waadilifu kunyima watuhumiwa dhamana.

"Imekuwa ni kama mchezo mtu anapelekwa mahakamani, anasomewa mashtaka, ananyimwa dhamana akiambiwa kwamba kosa husika halina dhamana anapelekwa kumande...miaka mitano nyuma kuna watu wameumia sana, waliwekwa ndani bila kisikilizwa, wamepigwa faini, familia zao zimesambaratika, wengine wamekufa kwa sababu ya makosa ambao mahakama ingeweza kuamua kama wanamakosa ama hawana," alisema.

Alisema DPP alitumia mwanya huo kushtaki wafanyabiashara na kuwanyima dhamana kinyume cha taratibu za Sheria ya Kodi inayoruhusu mazungumzo kati ya mlipakodi na kamishna wa kodi.

Alisema baada ya kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kwa kosa la kushindwa kulipa kodi, wafanyabiashara hao waliitwa na DPP kutaka plea-bargaining, kinyume cha taratibu.

# LHRC yalia na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimeibua hoja sita zinazopinga Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kwa lengo la kumnusuru mtoto wa kike dhidi ya madhara yanayotokana na ndoa za utotoni.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kijitonyama, Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema wanasikitishwa na mijadala kuhusu umri wa mtoto wa kike kuolewa.

Henga alikuwa akitoa tamko la kituo hicho la kukemea ndoa za utotoni na kusema; "Mijadala hii inapingana na sheria kwani baada ya Mahakama ya Rufani kuamua shauri la Rebeca Gyumi umri wa mtoto wa kike kuolewa Tanzania ni miaka 18 sasa. Ikumbukwe mahakama ni sheria lazima iheshimiwe na watu wote ikiwamo serikali," alisema Henga.

Alifafanua kuwa mijadala hiyo imekuwa ikitolewa kwenye vyombo ya habari na mitandao ya kijamii, ikipendekezwa kuwa hakuna haja ya kufanyia marekebisho sheria ya ndoa inayoruhusu umri wa ndoa kuwa miaka 14 kwa amri ya mahakama na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi, katika vifungu vyake vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Kutokana na mkanganyiko huo, LHRC inatoa mapendekezo sita, la kwanza likiwa ni umri wa kuolewa Tanzania uwe miaka 18 kulingana na kesi ya Rebeca Gyumi baada ya muda waliopewa serikali kurekebisha sheria kuisha.

"Tunapendekeza serikali irekebishe vifungu vya 13 ma 17 vya sheria ya ndoa ili kuonyesha nia njema (political will) na kuondoa upotoshaji wa umri wa ndoa kwa Watanzania," alisema.

Aidha, katika pendekezo la tatu, kituo hicho kinaziomba mamlaka na wadau kutumia nafasi zao kuunga mkono juhudi za kupambana na mila kandamizi zinazomnyima mtoto wa kike haki zake za msingi.

"Lakini katika pendekezo letu la nne, tunawaomba wadau wajiepushe matamko yanayorudisha nyuma juhudi za kumkomboa mtoto wa kike. Pendekezo la tano ni kutaka jamii kutambua kuwa mtoto wa kike ana haki za msingi, zilindwe na pia ijiepushe na desturi na mila zilizopitwa na wakati, kwani kufanya hivyo ni kuendelea kumkandamiza mtoto wa kike,"alisema.

Katika pendekezo lao la sita, Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema ni kuiomba serikali iondoe sheria zote kandamizi na kuhakikisha ulinzi wa mtoto kisheria unapatikana katika sheria zote za msingi katika ulinzi wa mtoto.

"Ukweli ni kwamba, ndoa za utotoni zimeendelea kuleta madhara makubwa kwa watoto wa kike na taifa kwa ujumla na kuendelea kusababisha hasara kwa taifa na baadhi ya hasara hizo ni kupoteza fursa ya elimu," alisema.

Alitaja nyingine kuwa ni maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU), magonjwa ya zinaa, kunyanyasika kisaikolojia, kimwili na kijinsia kupitia ukatili na kwamba mabinti katika vikwazo hivyo.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema ni wakati sasa kila mmoja kwa nafasi yake kupaza sauti ili kuwaokoa mabinti dhidi ya ndoa hizo, ili waondokane na vifo vya watoto wachanga na watoto wa kike pindi wanapojifungua, kwa kuwa viungo vyao vya uzazi havijakomaa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Dk. Anna Henga, akisoma tamko la kituo hicho, Dar es Salaam jana kulaani ndoa za utotoni na kuitaka serikali ifanye marekebisho ya vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Kulia ni Ofisa Mwandamizi Jinsia wa kituo hicho, Getrude Dyabene. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kamati ya Bunge yasema China ina uhusiano Afrika kimaadili pande zote

**Na Mwandishi Maalum**

MWENYEKITI wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ya Bunge la Tanzania, Vita Kawawa, amesema misingi ya China ya uaminifu, matokeo halisi, mshikamano na imani njema, pamoja na kujitolea kwake kwa maslahi makubwa zaidi na ya pamoja sio tu kanuni na maono ya kuendeleza uhusiano na nchi za Afrika, bali pia ni maadili ya pamoja ya Afrika na China.

Kawawa aliyasema hayo alipohudhuria kongamano la maadhimisho ya miaka 10 tangu Rais Xi Jinping wa China afanye ziara ya kiserikali nchini Tanzania na kuanzishwa kwa kanuni na dhamira zilizotajwa hapo juu. Kongamano hilo lilifanyika liliandaliwa na Ubalozi wa China nchini Tanzania.

"Chini ya mwongozo wa kanuni na dhamira, China na Tanzania zimefanya ushirikiano wenye tija, na kuleta manufaa yanayoonekana kwa Tanzania," Kawawa amesema, huku akielezea matarajio yake kuwa uhusiano wa nchi hizo mbili utapata maendeleo makubwa, na kuleta manufaa zaidi kwa watu wa nchi zote mbili.

Kwa mujibu wa Tovuti ya Gazeti la Umma la China, maofisa wengine wa Tanzania waliohudhuria kongamano hilo pia wameeleza kuwa kanuni na dhamira hizo zinathibitisha kuwa China ni rafiki wa dhati ambaye nchi za Afrika zinaweza kumwamini na kumtegemea.

Chen Mingjian, Balozi wa China nchini Tanzania, alifafanua maana ya msingi, thamani, umuhimu wa kihistoria, utendaji na mafanikio ya kanuni hizo za China katika uhusiano wake na Afrika.

"China iko tayari kushirikiana na Tanzania kutekeleza kwa pamoja Pendekezo la Maendeleo ya Dunia, Pendekezo la Usalama wa Dunia na Pendekezo la Ustaarabu wa Dunia, na kukuza uhusiano wa wenzi wa ushirikiano wa kimkakati wa pande zote kati ya China na Tanzania kuelekea siku nzuri za baadaye.

## Viongozi wa dini waombwa kutoa elimu ukatili wa kijinsia

**Na Denis Mambya**

VIONGOZI wa dini wameombwa kuelimisha jamii ili kuepusha vitendo vya ukatili wa kijinsia baada ya wengi wao kushindwa kuripoti matukio hayo polisi na mamlaka husika.

Ombi hilo lilitolewa jana na Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Morogoro, Jesca Kagunila, wakati akitoa takwimu za matukio ya ukatili wa kijinsia katika mkoa huo kwa mwaka 2022.

Alisema jumla ya matukio 5,125 yamebainika kutokana na mfumo wa ukusanyaji taarifa katika vituo vya afya mkoani humo.

Aidha, kati ya matukio 5,125 ya ukatili wa kijinsia kihisia ni 2,848, kimwili 1,748, kingono 529 na matukio yaliyopatiwa ushauri nasaha ni 2,843 sawa na asilimia 55.

Matukio yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi 1,397 sawa na asilimia 27 na yaliyopatiwa msaada wa kisheria yakiwa 583 sawa na asilimia 11.

Alisema kati ya halmashauri tisa za Mkoa wa Morogoro, nne ziliongoza kwa idadi kubwa ya matukio ya ukatili wa kijinsia, Kilosa ikiripotiwa matukio 1,192, Mvomero (1,138), Ifakara (1,127) huku Mlimba ikiripotiwa matukio 418.

Moses Mdemwa, mchungaji wa Kanisa la EAGT Nazareti, Kata ya Mkundi, Manispaa ya Morogoro, alisema watu kutokuwa na hofu ya Mungu ndiyo sababu ya ukatili wa kijinsia kuongezeka na kuwataka wamrudie Mungu na kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia katika mamlaka husika.

Othman Ally, kiongozi wa Masjid-bilal, Kata ya Mkundi alisema dunia ya sasa watu hawamwogopi Muumba wao bali huangalia yanayowapasa hapa duniani, kuna haja ya watu kubadilika katika mitazamo ya woga na kufichua kwa kuripoti matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

Beatrice Hussein, mkazi wa Kata ya Kihonda alisema watu wengi wanashindwa kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia kwa kuwa wengi wanaotenda ukatili ni ndugu na kuhofia kumripoti baba, mjomba au ndugu wa karibu ili undugu usipotee.

Ally Kassim Ally, mkazi wa kata ya Kihonda alisema kutokuwa na elimu ya ukatili wa kijinsia kunachangia ongezeko la ukatili, kwa kuwa wengi hushindwa kuripoti vitendo hivyo katika vituo vya Polisi kwa kutokuelewa madhara yatokanayo na ukatili yakiwamo ya kisaikolojia na kiafya.

Hata hivyo, umasikini umetajwa kuwa sababu kubwa ya ongezeko la vitendo vya ukatili wa kijinsia kutokana na uchunguzi uliofanywa kupitia ofisi ya ustawi wa jamii mkoa wa Morogoro.

HABARI KITAIFA

# TCCIA yataka w'biashara kujiunga 'Rupee Vostro'

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), kimewataka wafanyabiashara wa Tanzania kutumia akaunti maalum ya Rupee Vostro (SRVA) ambayo imeanzishwa kwa ajili ya shughuli za kibiashara na kukuza biashara ya kimataifa kati ya India na Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa TCCIA, Nebart Mwapwele, alisema hayo jana katika mkutano wa wadau wa biashara ya fedha za ndani ambao uliandaliwa na Ubalozi wa India nchini Tanzania.

Alisema hivi sasa waagizaji na wasafirishaji kutoka nchi zote mbili wanahimizwa kulipia bidhaa kwa sarafu zao baada ya SRVA kutambulishwa Benki Kuu ya India kwa miamala ya kibiashara.

Mwapwele alizipongeza serikali hizo kwa kuchukua hatua hiyo kwa sababu kuongeza thamani ya fedha, kupunguza gharama za uagizaji na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi, kuvutia wawekezaji kutoka nje na kuongeza ukuaji wa uchumi.

Alisema Tanzania na India ni marafiki wakubwa na bidhaa za nafaka, korosho zinauzwa nchini humo.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, alisema matumizi ya fedha hizo yameanzishwa na Benki Kuu ya India na kutoa wito kwa wafanyabiashara wa Tanzania kutumia fursa hiyo.

Alisema serikali ya India kupitia Benki Kuu imeondoa tozo ya fedha ili kuruhusu waagizaji na wasafirishaji wengi kupunguza gharama za ununuzi wa bidhaa, kuongeza mauzo ya nje na kuagiza baina ya nchi hizo na kukuza biashara ya kimataifa.

Pia alihamasisha benki za Tanzania kutumia fursa ya kwenda kufungua matawi yao India au akaunti maalum ya Rupia Vostro (SRVA) ili kuruhusu wafanyabiashara wa Tanzania kufanya miamala ya kibiashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Baroda Ltd, Aditya Narayan Singh, alisema hiyo ni mojawapo ya jitihada za RBI, kukuza ukuaji wa biashara ya kimataifa kwa kutilia mkazo katika mauzo ya nje na uagizaji.

# Zaidi ya walimu 10,000 wajengewa uwezo ufundishaji, umahiri

**Na Devota Mwachang'a**

MRADI bunifu wa elimu wa Shule Bora umefanikisha kuwajengea uwezo walimu zaidi ya 10,000 kwa kuwapa mafunzo kuboresha ufundishaji na umahiri katika baadhi ya mikoa unapotekelezwa mradi huo ndani ya mwaka mmoja.

Shule Bora ni mradi wa elimu wa serikali unaofadhiliwa na serikali ya Uingereza kupitia mfuko wa UK aid, unaotekelezwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika mikoa tisa nchini kwa msaada wa kiufundi kutoka Cambridge Education, ADD international, International Rescue Committee na Plan International.

Maelezo hayo yametolewa na Mratibu wa mradi kutoka TAMISEMI, Winfrid Chilumba, alipokuwa akitoa tathmini ya mwaka mmoja wa utekelezwaji wa mradi huo katika semina ya kuwapa uelewa wahariri na waandishi wa habari iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

"Mradi huu umefanikisha umekuwa chachu ya kuboresha elimu kwenye mikoa tisa ambao walimu wengi wemepata mafunzo wakiwamo 6,937 ambao wamejifunza kuibua hadithi za mafaniko za kujifunza za mfano ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji katika halmashauri 29 za mikoa ya Pwani, Katavi, Kigoma na Singida," alisema.

Pia, jumla ya walimu 4,944 kutoka halmashauri 19 za mikoa saba inakotekelezwa mradi wamefundishwa kuhusu miongozo ya mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) na wengine 944 wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika machakato wa ufundishaji.

Alisema walimu 1,747 wa elimu ya awali, darasa la kwanza na la pili, wawezeshaji rika na viongozi wa elimu ngazi ya mikoa, halmashauri, kata na shule katika mikoa ya Rukwa, Pwani, Simiyu, Mara, Dodoma na Tanga nao walipewa mafunzo.

Naye Godfrey Mulongo, naibu kiongozi wa timu ya mradi wa Shule Bora kutoka Cambridge Education Tanzania (CETL) ameeleza kuwa kabla ya kuanza utekelezaji walianza kwa kujenga msingi wa mradi, kuhakikisha mradi wa Shule Bora unakidhi mpango kazi na vipaumbele vya serikali katika kuboresha elimu.

"Tulianza na kuweka mipango kwa kuwapatia mafunzo walimu kupitia MEWAKA kuhakikisha walimu wanatatua changamoto ya kumudu Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto, na kuwaongezea elimu walimu ili wawaze kuwa wabobezi katika somo la Kiingereza," alisema Mulongo.

Mradi huo unatekelezwa kwa miaka saba (2021-2027) kwenye mikoa ya Rukwa, Pwani, Simiyu, Mara, Dodoma, Katavi, Kigoma, Singida na Tanga, mikoa hii ilipendekezwa na TAMISEMI baada ya kugundulika haifanyi vizuri kielimu kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo za utoro, mdondoko wa wanafunzi, idadi hafifu ya uandikishwaji wa watoto kuanza shule.


## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD na STEAM GENERATION RECOVERIES LTD,** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GAIMO CONSTRUCTION COMPANY LIMITED | GAUDENCE VINCENT LYMO AND MONICA GAUDENCE LYMO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI No.21393, L.O No.252865 | PLOT No. 407, BLOCK 'JJ', SITUATED AT OLOIRIEN, IN ARUSHA MUNICIPALITY | 13/04/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 2 | PRIMUS M TARIMO | LILIAN MWAKILASA ATHANAS | NYUMBA YENYE HATI MILIKI No.42315, L.O No. 313307 | PLOT No. 61, BLOCK ' ', SITUATED AT SOKONI 1, IN ARUSHA CITY | 14/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 3 | NESERIAN N GODSON | NOEL GODSON MEMURITI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO, S/MTAA | OLEVOLOSI STREET,KIMUNYAKI WARD IN ARUMERU DISTRICT | 15/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 4 | SAWE ADAM NASSARY | SAWE ADAM NASSARY | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO, S/MTAA | ILKILORIT STREET, MOIVO WARD IN ARUSHA DISTRICT | 15/04/2023, SAA 6:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 5 | EMMANUEL ANAEL OWISO | EMMANUEL ANAEL OWISO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO, S/MTAA | MTAA WA TEGETA A, KATA YA GOBA ,WILAYA YA UBUNGO DSM | 14/04/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 6 | MARY AFANDE MWAIPOPO | MARY AFANDE MWAIPOPO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK012270 | ARDHI No. TMK/MKW/MAK9/129, MAKANGARAWE, MANISPAA YA TEMEKE | 05/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 7 | JOHSNOM JOHN AKYOO | JOHSNOM JOHN AKYOO MUSHI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND029251 | ARDHI No. KND/KWE/KMZ7/147, MZIMUNI, KAWE, MANISPAA YA KINONDON. | 03/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD**
**P. O. Box 12943, Arusha**
**Tel: 0752632033 / 0628512033**

**STEAM GENERATION RECOVERIES LTD**
**P. O. Box 80607, Dar es Salaam**
**Tel: +255 715 91 74 51**

217345002

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Ni wakati mwafaka kuwapo mabadiliko Sheria ya Ndoa*

**WADAU** mbalimbali yakiwamo mashirika ya kutetea haki za binadamu, kwa siku kadhaa sasa, wamekuwa wakipaza sauti kuhusu kufanyiwa mabadiliko kwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 huku wakihoji usiri uliogubikwa katika kuharakisha mchakato huo kwa lengo la kumlinda mtoto wa kike.

Juzi, zaidi ya asasi zisizo za kiserikali 100 zilikutana ikiwa sehemu ya harakati za kutaka sheria hiyo ibadilishwe huku akihoji kuna kigugumizi gani kwa serikali katika kuifikisha bungeni sheria hiyo kwa ajili ya kufanyiwa mabadiliko. Sheria hiyo inatamka kuwa mtoto wa kike anaweza kuolewa akiwa na umri wa miaka 15 kwa kibali cha mahakama na miaka 15 kwa idhini ya wazazi.

Aidha, jana Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LRHC) jana kilikoleza mwangwi kwamba sheria hiyo ni kandamizi na inakiuka haki ya mtoto kwa kutamka kwamba anaweza kuolewa chini ya umri wa miaka 18. Kituo hicho kimepinga wazi sheria hiyo kuwa ni kandamizi, hivyo ni wakati mwafaka wa kuifanyia mabadiliko ili kumnusuru mtoto wa kike dhidi ya madhara yanayoweza kumpata hususan ndoa za utotoni.

Kwa ujumla sheria hiyo inapingana na ile ya haki ya mtoto inayotoa ufafanuzi kwamba mtoto atahesabika kuwa ameondoka au kuvuka katika kundi hilo baada ya kufikisha umri wa miaka 18.

Wanaharakati hao na wadau wa haki za binadamu, hususani za watoto, wamepaza sauti hizo baada ya hivi karibuni mmoja wa viongozi wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kutoa maoni mbele ya Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Haki Jinai kwamba Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ibaki kama ilivyo na kwamba kwa mujibu wa dini yao, mtoto anaweza kuolewa baada ya kuvunja ungo hata kama ana umri wa miaka 10, 12 au 13!

Itakumbukwa kwamba mwaka 2016, Shirika la Msichana Initiative kupitia mkurugenzi wake, Rebecca Gyumi, lilifungua kesi kupinga vifungu vya 13 na 17 vya sheria hiyo lakini serikali ilikata rufani na kushindwa baada ya Mahakama ya Rufani kukubali kwamba vifungu hivyo vinapingana na Katiba ya nchi kwa kuweka umri tofauti wa kuolewa kati ya mtoto wa kike na kiume.

Wahenga wanasema panapofuka moshi pana moto, hivyo sauti hizi zinazopazwa na wanaharakati hao zinapaswa kuchukuliwa kwa uzito unaostahili kwa sheria hiyo kufanyiwa mabadiliko.

Serikali inapaswa kukubali kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo ili kuondoa ukinzani wa sheria mbili tofauti ilizozitunga zenyewe. Kwa muungwana kukubali kwamba kuna kosa mahali si jambo baya, hivyo serikali ikubali mabadiliko hayo kwa manufaa ya taifa katika kuwalinda watoto.


Ni dhahiri kwamba katika nyakati za sasa, mtoto wa kike hadi anafikisha miaka 18 anakuwa bado anaendelea na masomo, hivyo kuiacha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 iendelee kutumika hasa vifungu vinavyoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 au 15, ni ukiukwaji wa haki ya mtoto ya kupata elimu.

Inawezekana kwamba wakati sheria hiyo inatungwa mwaka 1971 watoto wengi wa kike walikuwa hawapewi nafasi kupata elimu kama ilivyo kwa wa kiume lakini sasa kuna suala la usawa wa kijinsia na wanawake wamepewa nafasi kubwa katika masuala ya elimu na uongozi katika serikali, taasisi zake na mashirika ya umma na binafsi.

Kutokana na kuwapo kwa hoja za wadau katika harakati za kuwalinda watoto wa kike dhidi ya ndoa za utotoni, ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kukaa na wadau hao kupitia asasi za kutetea haki za binadamu pamoja na viongozi wa dini kukaa pamoja na kufanya mabadiliko kwa kufuta vifungu kandamizi dhidi ya watoto kwa ustawi wa watoto na taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

## *Hongera Marekani kulisha wanafunzi*

**KARIBU** Makamu wa Rais Kamala Harris. Ujio wako ni muhimu hasa kwa sababu kuna mengi yanayofanyika kwa msaada wa Marekani na yapo ya kujifunza zaidi.

Mataifa hayo yanashirikiana na kukuza taaluma kupitia mpango wa kutoa chakula shuleni, ambao mwishoni mwa mwaka jana serikali za nchi hizo zilizindua mradi wa elimu na lishe, programu iliyopewa jina la 'Pamoja Tuwalishe'.

Uzinduzi wa mradi huo ulifanyika katika hafla maalumu, jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde na Prof. Bonaventure Rutinwa ambaye in Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyewakilisha Wizara ya Elimu.

Aidha, kwa upande wa serikali ya Marekani, iliwakilishwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Jewel Bronaugh na Kaimu Balozi wa Marekani nchini Robert Raines, ambao wanaeleza kuwa programu hiyo itainua ufaulu wa wanafunzi watakaoshiriki na kufungua zaidi fursa zao siku za usoni.

Mradi huo unatarajiwa kunufaisha zaidi ya Watanzania 355,000 wakiwamo wanafamilia, walimu, wakulima na wanajamii kwa kuboresha taaluma kupitia utoaji wa chakula kwa wanafunzi shuleni.

Kimsingi, kuna umuhimu na thamani kubwa ya programu hiyo ya kimataifa ya lishe shuleni, kutokana na ukweli kwamba katika maeneo mengi wanafunzi wanashinda njaa na kushindwa kufanya vizuri katika masomo.

Hivyo, mradi huo ungepaswa kuongeza ari kwa wazazi kuona umuhimu wa kuchangia chakula shuleni, kwa kupanua wigo badala ya maeneo machache ambayo mradi huo umeelekezwa, bali nchi nzima.

Programu ya Kimataifa ya Lishe Shuleni ya McGovern-Dole inaendeshwa nchini na inaelezwa kuwa ari ya Wizara ya Kilimo ya Marekani kuusaidia ni kubwa hivyo ni muhimu kuunga mkono juhudi hizo.

Ikumbukwe kuwa, Wizara ya Kilimo ya Marekani imekuwa ikitoa msaada wa kiufundi, kifedha na kimawazo kwa programu za chakula shuleni na elimu tangu mwaka 2010, hivyo juhudi hizo ni sehemu ya mafanikio ya ushirikiano ambayo Mama Kamala Harris atafurahi kukutana nayo.

Ninaamini kwamba si rahisi wadau hao kufika maeneo yote ya nchi, hivyo wazazi na walezi nao ni muhimu wafanye sehemu yao kuhakikisha watoto wao wanapata chakula shuleni badala ya kushinda njaa.

Kumekuwapo na mawazo mtazamo unaokinzana kuhusu kuwapo kwa chakula shuleni, hasa baada ya serikali kuamua kutoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha sita.

Wapo wazazi na walezi wanaoamini kwamba suala la chakula shuleni ni jukumu la serikali, hivyo hata kama wana chakula cha kutosha, hawako tayari kukitoa, ili watoto wao wakale shuleni.

Kesho Tanzania itakuwa na ugeni mkubwa wa Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris ambaye amekuwa na ziara ya wiki moja Afrika akianzia nchini Ghana.

Marekani imekuwa ikiisaidia Tanzanaia katika miradi mbalimbali mojawapo ukiwa ni huo wa lishe shuleni, kwa ajili ya kusaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi watakaoshiriki na kufungua zaidi fursa zao katika siku za usoni.

Kwa kuwa mradi huo upo sehemu chache, ninadhani ujio wa Makamu wa Rais wa Marekani, ungetuamsha Watanzania hasa wale ambao wamekuwa hawaoni umuhimu wa kuchangia chakula shuleni, wabadalike.

Wizara ya Elimu imekuwa ikieleza kuwa mwanafunzi asipopata chakula shuleni, anakosa usikivu wakati wa kujifunza, mambo hayaingii akilini, aidha mahudhurio huwa hafifu na utoro na mwisho wake ni kukatisha masomo.

Kutokana na umuhimu wa chakula shuleni, wizara ilishazindua Mwongozo wa Kitaifa ya Utoaji Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa elimu msingi kwa lengo la kuwaelekeza wadau wa elimu bora ya kutekeleza utoaji huduma ya chakula na lishe kwa wanafunzi.

Lakini ombi linawaangukia wadau wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali, kampuni binafsi na vyombo vya habari kuendelea kushirikiana na serikali ili wanafunzi wapate chakula wanapokuwa shuleni.

Ingependeza iwapo kila mmoja atafanya sehemu yake ili shule ziwe na chakula, jamii isiwaachie wahisani tu wakiwamo Wamarekani na wengine wachache, bali kila mmoja kuhusika kuwasaidia wanafunzi katika hilo.

# Masomo ya NBAA sasa kidijitali duniani kote

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), imenunua mtambo wa kisasa wa kufundishia mtandaoni ambao utawawezesha watu kusoma kokote waliko duniani na kufanya mitihani mtandaoni.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, CPA Pius Maneno, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mtambo huo uitwao 'NBAA Training Infrastructure', ulionunuliwa nje ya nchi kwa gharama ya Sh. milioni 150.

Uzinduzi huo ulishuhudiwa na Rais wa Shirikisho la Wahasibu Afrika (PAFA), Cosme Goundete, raia wa Benin na Makamu wake, Keto Kayemba, raia wa Uganda na Mtendaji Mkuu wa PAFA, Alleta Prinsloo, na wajumbe 28 wa shirikisho hilo kutoka mataifa mbalimbali.

Alisema NBAA ilichukua uamuzi wa kununua mtambo huo kutokana na malalamiko sehemu mbalimbali kwamba wanataka kufanya mitihani ya bodi hiyo lakini wanakaa mbali na Dar es Salaam na wengine nje ya nchi.

"Mtu anakwambia niko Kigoma au Mtwara nataka kufanya mitihani yenu nafanyaje? Sasa hali hii imetupa changamoto ya kutafuta mtambo huu na sasa mtu yeyote duniani anaweza kufanya mitihani ya NBAA akiwa nchi yoyote ile," alisema.

Maneno pia alisema wiki hii kutakuwa na kikao cha siku mbili cha (PAFA na kwamba kitahudhuriwa na wajumbe 28 kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika, wakiwamo wengine waliokuja kuwa watazamaji kutoka Marekani na Ulaya.

Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude, aliipongeza NBAA kwa uamuzi wake wa kununua mtambo huo kwani utawarahishia wanafunzi wengi kusoma bila kulazimika kwenda Dar es Salaam na kufanya mitihani hiyo.

"Haya ni mapinduzi makubwa kwa sababu si tu kwamba mtambo huu utaokoa gharama za kusafiri lakini pia utatatua changamoto ya watanzania wengi wanaofanya kazi nje ambao ni wanachama wa NBAA namna ya kupata mafunzo kwani walilazimika kupanda ndege kuja NBAA lakini sasa watafanyia huko huko," alisema.

Mkude alisema mtambo huo utasaidia kuongeza idadi ya watu wanaosomea fani ya uhasibu kwani hakutakuwa na gharama ya kupanda ndege kuja kusoma hapa nchini kama ilivyokuwa.

Alisema fani ya CPA inaheshimika sana duniani, hivyo Watanzania na watu kutoka nje wenye kuhitaji mafunzo yanayotolewa na NBAA watachangamkia fursa ya kuwapo kwa mtambo huo na kupata kile wanachokihitaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya NBAA, Prof. Sylivia Temu, alisema kupitia mafunzo hayo kwa njia ya mtandao anaamini kwamba wataweza kuwafikia wadau wao wa nje na ndani ya nchi ambao walitamani kusoma kwenye bodi hiyo lakini walikuwa wanakwamishwa na umbali.




Mkurugenzi wa Kampuni ya NALA, Benjamin Fernandes (katikati), akionyesha leseni ya mtoa huduma kwa malipo, baada ya kukabidhiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kwenye mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Meneja bidhaa wa kampuni hiyo, Thomas Robinson na Mtaalamu wa Programu, Bertha Sanga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Naibu Waziri ataka programu bora kuboresha utendaji utumishi umma

**Na Mwandishi Wetu**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete amekitaka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) na Taasisi ya Uongozi kuandaa programu za mafunzo zitakazowajengea uwezo kiutendaji watumishi wa umma na viongozi.

Kwa kufanya hivyo, amesema watakuwa na uwezo wa kutoa huduma bora kwa wananchi na mchango katika maendeleo ya taifa.

Kikwete (pichani) alitoa maelekezo hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa ziara yake ya kikazi katika TPSC na Taasisi ya Uongozi iliyolenga kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa taasisi hizo.



Alisema watumishi wa umma na viongozi katika taasisi zote za umma wanahitaji kupata mafunzo yenye tija kwa ajili ya kukuza taaluma na kuongeza ufanisi kiutendaji. Kutokana na umuhimu huo, alisema taasisi hizi zinapaswa kuhakikisha watumishi na viongozi wanapata mafunzo yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Kikwete alisisitiza kuwa TPSC inatoa mafunzo kwa watumishi ambao wameshaajiriwa na serikali, hivyo wanahitaji kuandaliwa programu nzuri za mafunzo zitakazoimarisha utendaji kazi wao.

Sambamba na hilo, Kikwete aliipongeza TPSC kwa kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma wanaokaribia kustaafu ili kuwaandaa wawe na maisha mazuri baada ya kustaafu kuutumikia umma.

"Binafsi naamini Chuo cha Utumishi wa Umma mnafanya jambo zuri kuwapatia mafunzo watumishi wanaokaribia kustaafu kwa mujibu wa sheria. Mkijipanga vizuri nina uhakika hawataharibikiwa pindi watakapostaafu," alisema.

Akizungumza na menejimenti ya Taasisi ya Uongozi, Kikwete aliiagiza taasisi hiyo kubuni programu za mafunzo ambazo zitawaandaa viongozi wa baadaye, kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amekusudia.

Kikwete alisema Rais Samia anatamani kuona Taasisi ya Uongozi inatoa mchango wa kuwaandaa viongozi watakaoendeleza kazi nzuri iliyofanywa na uongozi wake.

## KABWELA



# Bima mazao yaanzishwa kufidia wakulima

**Na Gwamaka Alipipi**

KILIO cha wakulima kuhusu hasara ya mazao inayotokana na majanga, kimepata jibu baada ya kampuni ya Yara Tanzania kuzindua bima ya mazao itakayowalinda dhidi ya hasara hiyo kunakosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Kampuni hiyo kupitia mpango wake uitwao Africaconnect, ilizundua huduma hiyo jana jijini Dar es Salaam na kwamba itakuwa inatoa bima ya mazao kupitia kampuni ya bima ya Jubilee.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema kutoa bima ya mazao kwa wakulima ni hatua kubwa. Alisema lengo kuu ni kuwawezesha wakulima kupata riziki yao pamoja na kulinda usalama wa chakula.

"Kwa kujiunga na Africaconnect, kampuni ya Jubilee Insurance imeongeza msukumo wa kufanya kilimo Tanzania kuwa thabiti na chenye faida," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema washirika wengine katika mchakato huo ni Benki ya Equity, Corteva Agriscience, Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendeshaji Mbegu za Kilimo na Kampuni ya Murzah Wilmar Rice Millers Ltd.

Alisema Jubilee Insurance imekuwa mshirika mpya katika kujiunga na mpango huo unaotoa suluhisho la uhakika katika kuongeza tija kwa wakulima.

Odhiambo alisema wakulima wanaopenda kujiunga na mpango huo wanaweza kufanya hivyo kwa kuwatumia mawakala wa mbolea wa Yara walio karibu nao au tawi lolote la Benki ya Equity.

Ofisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Jubilee Insurance, Dipankar Acharya, alisema: "Tumefurahi kuwa washirika wa Africaconnect ili kuwalinda wakulima na hasara za mazao zinazosababishwa na majanga ya asili kwa kuwapa bima ya mazao na ushughulikiaji bora wa hatari wanazokabiliana nazo katika kilimo".

Alisema kupitia mpango huo wakulima wataweza kulima kwa matumaini, mafanikio pamoja na kuwainua kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Equity, Isabela Maganga, alisema mwaka jana walitoa mkopo wa Sh. bilioni 1.1 kwa wakulima 1,400 wa mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Arusha, Manyara na Iringa kupitia mpango wa Africaconnect.

Maganga alisema: "Umekuwa mwaka wa furaha kwa ushirikat wetu huku wakulima wakipata mikopo ya pembejeo isiyo na dhamana kutoka benki yetu. Tunatarajia kuwahudumia wakulima wengi zaidi mwaka huu Yara inapotanua wigo wa huduma kwa kuingiza mazao mengi zaidi katika mpango huu."



Ofisa Tawala wa Wilaya ya Ilala, Dar es Salam, Charangwa Selemani (kushoto), akiangalia bidhaa za mjasiriamali wa vitenge, Editha Julius (kulia), alipotembelea maonyesho wakati wa uzinduzi wa programu atamizi ya biashara ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) jana. Kushoto kwake ni Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yahamasisha vijana kujiunga programu atamizi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewahamasisha vijana kujiunga na programu atamizi inayotolewa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), ili wapate ujuzi wa biashara na hatimaye kuwa wafanyabiashara wazuri wanapomaliza elimu ya vyuo.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara katika Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Sempeho Manongi, wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa siku ya programu atamizi chuoni hapo.

Uzinduzi huo uliofanywa na Ofisa Tawala wa Wilaya ya Ilala, Charangwa Selemani na unalenga kuwawezesha wanafunzi wenye mawazo ya biashara kuyakuza na hatimaye kuwa wafanyabiashara wakubwa.

Alipongeza hatua ya chuo hicho kuanzisha programu hiyo akisema inaleta uhalisia zaidi kuliko masomo ya nadharia na kwamba itawasaidia sana wanafunzi wa chuo hicho kupata ujuzi wa biashara.

"Nafurahi kuona CBE imesimama kwenye misingi ya kuanzishwa kwake kwa kuanzisha programu kama hii ya atamizi ambazo zitakuwa na matokeo ya haraka sana kuliko nadharia, mnatakiwa kuishi kwenye maisha ya watu ya sasa ili waweze kujiajiri na kwa hili mmefanikiwa.

"Natamani mboreshe zaidi ili vijana wengi wanaomaliza hapa CBE wawe wameshapata elimu ya ujasiriamali kama hii ambao sasa wataajiri vijana wengine wanaotoka kwenye vyuo mbalimbali," alisema Manongi.

Kaimu Mkuu wa CBE, Prof. Edda Lwoga, alisema chuo kiliamua kuanzisha programu hiyo atamizi ya biashara ili kuunga mkono juhudi za serikali na kimeendelea kuweka mipango mbalimbali madhubuti kuinua ubora wa chuo.

"Sisi CBE tumaanini hizi programu atamizi za biashara na teknolojia zitachangia kuibua na kulea ndoto za biashara za wanafunzi ili hata wakimaliza vyuo waendeleze biashara zao na kuajiri wengine," alisema Lwoga.

Alisema chuo hicho kilianza programu atamizi mwaka juzi na mwaka jana kilianza msimu wa kwanza na wanafunzi 100 kwenye programu hiyo na wengine wameshiriki kwenye maonyesho kuonyesha walivyofanikiwa katika kujiajiri wakiendelea na masomo.

Alisema chuo hicho kimewekeza kwenye atamizi ya biashara ili kuionyesha dunia kwamba wanatoa mafunzo kwa vitendo ili kupunguza tatizo la ajira nchini kwa wanafunzi wanaomaliza kujiajiri wenyewe.

Selemani alipongeza chuo kwa mawazo ya kuanzisha programu ya kuwalea na kuwakuza vijana wenye mawazo ya biashara mbalimbali.

"Mkurugenzi wa wizara amesema hapa kwamba mnaanza kurudi kwenye malengo ya kuanzishwa kwenu kwa kuwa kweli chuo cha biashara kinachofundisha kwa vitendo siyo nadharia tu kwa hiyo mnavyowanyanyua hawa mnatimiza lengo la kuanzishwa chuo," alisema.

Aliwapongeza wanafunzi waliomaliza programu hiyo mwaka jana na kuweza kuanzisha biashara mbalimbali huku akiwataka wanafunzi wengine kujiunga ili kutumia fursa hiyo kuinuka kibiashara.

Wajasiriamali wengi, alisema wanajifunza namna ya kuzalisha bidhaa mbalimbali hivyo wanatakiwa kwenda kutafuta masoko ya bidhaa zao na kuhakikisha wanazifungasha kitaalamu ili kuvutia wateja.

Alikitaka chuo kusaidia kuwafundisha wanafunzi wenye biashara namna ya kuingia na kushindana kwenye masoko na kuwaelimisha namna ya kuboresha bidhaa.

"Wengi mnataka mkimaliza shule mkaajiriwe ofisini lakini ajira ni kile kinachokuingizia kipato. Unakuta mtu anafanya biashara inamwingizia fedha nyingi lakini ukimuuliza unafanya kazi gani anakuambia sina ajira. Ondoeni mawazo ya kuajiriwa, nendeni mkajiajiri," alisema.

# Wazazi wasisitizwa watoto chanjo surua

**Na Elizabeth John**, NJOMBE

WAZAZI na walezi mkoani Njombe wametakiwa kuwapeleka watoto ambao hawakupata chanjo ya dozi ya kwanza na ya pili ili kujikinga na ugonjwa wa surua.

Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Njombe, Valerian Makasi, alisema jana kuwa tangu kuanza kwa kampeni hiyo Machi 6 hadi 26, mwaka huu, wamewafikia watoto 16,159.

"Awali kwa mujibu wa takwimu za Januari 2019 hadi Mei 2022, malengo yalikuwa kuwafikia watoto 12,827 ambao hawakupata chanjo. Hii ni kutokana na kuwapo kwa milipuko katika maeneo mbalimbali ukiwamo mkoa wetu wa Njombe kwenye Halmashauri ya Makambako.

Mkoa kwa kushirikiana na wizara tulijipanga tukaandaa kampeni kuhakikisha tunawatafuta watoto wote ambao hawajapata chanjo, wengine hawakukamilisha dozi na kuhakikisha tunawapa chanjo," alisema Makasi.

Alisema chanjo hiyo inatolewa bure na kwa njia mbalimbali kwa kupita nyumba kwa nyumba, maeneo ya biashara, mashambani na katika vituo vya kutolea huduma za afya.

"Tumekuwa tunahamasisha jamii, wazazi umuhimu wa chanjo hii kwa kutumia njia mbalimbali kama matangazo kwa njia ya magari, redio lakini pia kupitia mikutano mbalimbali ambayo imekuwapo kwenye jamii ili kuhakikisha wanajamii wanaelewa umuhimu wa chanjo na kuwapeleka watoto katika maeneo yaliyoainishwa kwenye vijiji vyao ili wapate chanjo," alisema.

Makasi alisema watoto wengi hawakupata chanjo awali kwa sababu ya mwingiliano wa ugonjwa wa UVIKO-19.

Mratibu wa Chanjo Halmashauri ya Mji wa Njombe, Simon Ngasa, alisema kinga ya ugonjwa wa surua ni kupata chanjo.





# Tanga UWASA kufufua visima vilivyoachwa bila uangalizi

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi Mazingira jijini Tanga (Tanga UWASA), imetangaza nia yake ya kuvifufua visima vyote vya maji vilivyochimbwa na serikali na kuachwa bila uangalizi ili visaidie kupunguza tatizo la uhaba wa maji linalotishia wananchi walio wengi.

Ofisa Mwandamizi wa Mamlaka hiyo, Salum Ngumbi, akizungumza jana na wateja na mabalozi wa maji waliotembelea miradi inayotekelezwa ili kujifunza na kupata elimu ya matumizi sahihi ya maji, alisema visima hivyo ni vilivyopo Uwanja wa Ndege na Mwakileo.

Alisema, vitatumika kama mbadala wa maji ya Tanga inapotokea yamepungua na kusababisha adha ya maji kwa wakazi wa jiji hilo.

"Mpango tulionao kwa sasa ni kuhakikisha kuwa wateja wetu wanapata maji ya kukidhi mahitaji muhimu. Tuna mpango wa kuanza miradi ya maendeleo hasa, mradi wa ujenzi wa kutanua Bwawa la Mabayani na tunatarajia uanze Septemba, mwaka huu," alisema Ngumbi.

Alisema pamoja na kufufua visima hivyo ni lazima watahakikisha wanaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi, ambao uwahudumia kila siku ili kuondoa vikwazo wanavyokutana navyo.

Upatikanaji wa maji kwa siku katika maeneo yote ni lita za ujazo 30,000, kwa sasa mpango ni kuongeza uzalishaji kufikia lita 45,000.

"Kwa sasa upo mradi uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni 10, fedha hizo ni kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika jamii, kwa sababu tunafanya hivi ili kuhakikisha yaliyojitokeza kwa wananchi kukumbana na tatizo la huduma ya maji hayajitokezi tena," alisisitiza.

Mtaalamu wa maabara katika mtambo wa kutibu maji wa Mowe, Amos Rwehangana, alisema kwa sasa hali ya kutoka kwa maji iko vizuri katika maeneo mbalimbali.

**Kwa sasa upo mradi uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni 10, fedha hizo ni kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika jamii, kwa sababu tunafanya hivi ili kuhakikisha yaliyojitokeza kwa wananchi kukumbana na tatizo la huduma ya maji hayajitokezi tena.**

# Hospitali yapunguza tatizo vifo vya watoto

**Na Jaliwason Jasson,** MBULU

HOSPITALI ya Rufani ya Kilutheri ya Hydom (HLH), inayotekeleza mradi wa kitita cha uzazi salama katika mikoa ya Manyara, Geita, Shinyanga, Mwanza na Tabora, imefanikiwa kuokoa watoto wenye umri chini ya siku moja na wanaozaliwa wafu, kupungua kwa asilimia 25.

Mkurugenzi wa HLH, Dk. Paschal Mdoe, alisema mradi huo wanautekeleza kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Chama cha Madaktari Bingwa Wanawake, Chama cha Madaktari Bingwa wa Watoto na Chama cha Wakunga.

**Katika vituo vyote vyenye mradi kuna mafanikio na watoto wameokolewa kwa asilimia 50 wenye umri chini ya siku moja na watoto wanaozaliwa wafu wamepungua kwa asilimia 25.**

"Mradi huu unatekelezwa katika vituo 30 kwenye mikoa hiyo, na kila mkoa una vituo sita. Mikoa hiyo ilichaguliwa kutokana na kuwa na vifo vingi vya kinamama na watoto wachanga, usipokuwa Manyara ilikuwa na vifo vichache," alisema.

Mradi huo ulioanza kutekelezwa Novemba 2020 katika mikoa hiyo mitano, ulitokana na Hospitali ya Kilutheri ya Haydom, kuandika andiko na kupata Dola za Marekani milioni 4.5, sawa na Sh. bilioni 11.

Alisema mradi unatekelezwa katika vituo 30 kwenye mikoa hiyo na kila mkoa una vituo sita, mikoa hiyo ilichaguliwa kutokana na vifo vingi vya kinamama na watoto wachanga.

Kwa mujibu wa Dk. Mdoe, tangu kuanza kwa mradi huo kuna mafanikio makubwa kwa watoto, ambao wanazaliwa wafu na watoto wanaokufa mapema ndani ya saa 24.

"Katika vituo vyote vyenye mradi kuna mafanikio na watoto wameokolewa kwa asilimia 50 wenye umri chini ya siku moja na watoto wanaozaliwa wafu wamepungua kwa asilimia 25," alisema.

Kutokana na mjongeo chanya wa mradi huo, Benki ya Dunia (WB), Mfuko wa Global Financing Facilities wanafadhili mradi huo, Serikali ya Norway na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), wameonyesha nia ya kuongeza Sh. bilioni 17 ili kuongeza vituo kufikia 140.



Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi ya Mpapayu wilayani Muheza, mkoani Tanga, Ally Chogogwe, akionyesha kwa waandishi wa habari juzi paa za madarasa yaliyochakaa na kuhatarisha usalama wa wanafunzi na walimu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mkoa wa Manyara waongeza idadi uandikishaji watoto darasa awali

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara, umepata mjongeo chanya katika uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na la kwanza mwaka huu, baada ya kuandikisha watoto 102,369.

Kiwango hicho ni cha juu na hakijawahi kutokea, hasa kutokana na mila na desturi za jamii za kifugaji.

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu Taaluma, Mkoa wa Manyara, Julitha Akko, mpaka uandikishaji huo unafika tamati, waliandikisha wanafunzi wa awali wavulana 24,885 na wasichana 23,367.

Wakati darasa la kwanza walioandikishwa, wavulana ni 27,397 na wasichana ni 26,720, sawa na asilimia 103.7

Alisema halmashauri za wilaya zenye idadi kubwa ya wafugaji zimefanya vizuri kwenye uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Vilevile, kutokana na madarasa ya awali katika kila shule ya msingi, imekuwa rahisi kuwaandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza, baada ya kufanya maoteo.

Suala la elimu ni la lazima kwa kuwa Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, inasisitiza watoto wote kuandikishwa shule na kuhudhuria masomo.

Kutokana na msukumo huo wa sheria, Akko, alisema ikitokea mzazi au mlezi akashindwa kumwandikisha mtoto wake, mahakama ndio inatoa adhabu kulingana na sheria.

Pia Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, inaelekeza kuwa serikali itaweka utaratibu wa elimu ya awali, kuwa suala la lazima kutolewa kwa watoto, kuanzia umri wa miaka mitatu hadi mitano kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja.



# Elimu ukatili kijinsia itolewe ngazi ya jamii

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWANASHERIA wa Shirika la Haki za Binadamu na Huduma za Kisheria (HLC), Pius Juma, amesema ili kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinisia nchini inatakiwa itolewe elimu ya mara kwa mara katika ngazi ya jamii ili kuelewa madhara ya kuwahifadhi watu wanaotekeleza ukatili huo kwa watoto na wanawake.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na gazeti hili na kusema wananchi waliopo pembezoni hawafikiwi na elimu ya ukatili wa kijinsia.

**Kituo kinaitwa One Stop Center ambapo kwa sasa kimesaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo na kinamama.**

Alishauri wadau kuzunguka katika maeneo korofi na kuhakikisha tatizo hilo linadhibitiwa katika ngazi ya jamii badala ya kukaa ofisini kusubiri kuletewa waathirika.

"Hii ni kazi ya kuanzia kwenye jamii ili tuweze kudhibiti kwanza wale wanaotekeleza ukatili maana mara kadhaa wamekuwa wakiwarubuni ndugu wa waathirika na kupoteza ushahidi hali ambayo inawapa kiburi na kuendelea kutenda vitendo hivyo," alisema Juma.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Msalala, Richard Ng'ondya alisema serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wanafanya juhudi kudhibiti vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na kuwahudumia watu waliofanyiwa ukatili.

Alisema katika halmashauri hiyo kipo kituo kinachopambana na vitendo vya ukatili kwa jamii kwa kuendelea kutoa elimu ya madhara ya vitendo hasa kwa wanaozungukwa na wachimbaji wadogo.

"Kituo kinaitwa One Stop Center ambapo kwa sasa kimesaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo na kinamama hususani wanaoishi jirani na machimbo ya wachimbaji wadogo," alisema Ng'ondya.

Alisema kituo hicho kimejengwa na shirika lisilo la kiserikali la Kiwohede linalotekeleza mradi wa ukatili wa kijinsia kwa thamani ya Sh. milioni 95 kwa ufadhili wa UNFPA, UN-WOMEN pamoja na KOICA na kinasimamia utoaji wa elimu ya vitendo vyote vya ukatili na madhara yake.

Alisema kituo hicho kimejengwa jirani na kituo cha afya cha Bugarama na kwa siku wanatoa huduma kwa waathirika 10 hadi 15 kinajumlisha na wanaofanyiwa vipimo baada ya kufanyiwa ukatili.

Ng'ondya alizitaja huduma zinazotolewa kuwa ni pamoja na Ofisi ya Dawati la Jinsia, Afya, Ustawi wa Jamii, Kamati ya Mtakuwwa ngazi ya kata pamoja na ofisi ya msaada wa kisheria ili inapotokea au kuripotiwa kwa kesi katika kituo iweze kushughulikiwa kwa haraka na wahusika wanawajibishwa kisheria.

Angelina Malembeka, mkazi wa Segese katika halmashauri hiyo alisema, walikuwa wamepoteza imani na ofisi za vijiji na kata kutokana na viongozi wake kusubiri kuletewa taarifa ofisini na wakati mwingine walikuwa wakitoa taarifa zinavujishwa na kuwarudia walengwa ambao walikuwa wanakimbia na kutokomea kusikojulikana.

## WAMACU waiangukia serikali uhakiki mali za ushirika

**Na Timothy Itembe,** MARA

CHAMA cha Ushirika wa Wakulima wa Mkoa wa Mara (WAMACU) wameomba serikali kuingilia kati mchakato wa kutambua na uhakiki mali za ushirika ili kuimarisha ushirika huo na kuwanufaisha wanachama wake.

Akizungumza ofisini kwake na waandishi wa habari, Meneja Mkuu wa ushirika huo, Sameli Gisiboye alisema mchakato wa kutambua na kuhakiki mali za ushirika ni umeanza hivyo ni vyema serikali ikashiriki katika uhakiki huo ili kudhibiti ubadhirifu pamoja na upotevu wa mali za ushirika.

"Hapo nyuma tumeshuhudia mali za ushirika zikipotea na kuhujumiwa, lakini kipindi hiki serikali imekuja na mpango wa kuimarisha ushirika kwa hali hiyo tunaomba kuungwa mkono wakati zoezi linaendelea la kutambua na kuhakiki mali za ushirika ili wanufaika waendelee kunufaika na ushirika," alisema Gisiboye.

Gisiboye alisema, mwaka huu wamepanga kupanua wigo na kuunganisha mazao yote ya kimkakati yakiwamo tumbaku na alizeti ambayo yanalimwa mkoani humo hususani wilaya Serengeti na kuhakikisha yanauzwa kwa kufuata sheria ili kuwanufaisha wakulima.

Awali, katika kikao hicho wakulima waliomba serikali kuwachukulia hatua kali wenye tabia ya kutorosha kahawa na kuuza nchi jirani ya Kenya wakitaja hatua hiyo kuwa ni makosa ya kisheria na kuomba watu wachukuliwe hatua.

Naye Kija Maheda, Mrajisi Mkoa Mara, alisema serikali imepanga kununua mazao kupitia AMCOS na wanunuzi wengine walioruhusiwa kisheria na kuwataka wakulima kutodanganyika na kuibiwa kahawa kwa kuwauzia walanguzi wa gorogoro na vipimo visivyo sahihi.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (kulia), akikagua baadhi ya vipuli vitakavyofungwa katika vivuko vinne vinavyofanyiwa ukarabati katika yadi ya Songoro mkoani Mwanza juzi. Vivuko hivyo ni MV Misungwi (Kigongo - Busisi), MV Mara (Iramba - Majita), MV Ujenzi (Kisorya - Rugezi) na MV Nyerere (Bugolora -Ukara). **PICHA: WUU**

## SIHAS kutoa wanafunzi kuelimisha magonjwa mlipuko

**Na Vitus Audax,** SUMVE

CHUO cha Afya Shirikishi Sumve (SIHAS), kimeweka mpango wa kuandaa na kupeleka wanafunzi wa chuo hicho katika maeneo mbalimbali ya vijijini kwa lengo la kutoa elimu ya magonjwa ya mlipuko kwa jamii isiyofikiwa na elimu hiyo ili kuwasaidia kukabiliana nayo yanapotokea.

Akizungumza na gazeti hili juzi kuhusu mipango yao katika kukabiliana na magonjwa hayo ikiwamo marburg, mkuu wa chuo hicho, Reuben William alisema, wameanza kuwaandaa wanafunzi ili kutoa elimu hiyo kwa jamii.

Kadhalika alisema kuelekea mwisho wa muhula wa masomo wameandaa vipeperushi kwa ajili ya kusambaza katika maeneo mbalimbali ya vijijini pamoja na wale wanaoelekea nyumbani kwao watapatiwa vipeperushi hivyo ili kuzidi kuwaelimisha wanafunzi kujikinga na magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na marburg.

William alisema wamefikia hatua hiyo baada ya kupokea utafiti uliofanywa na wanafunzi wa chuo hicho na kubaini kuwa idadi kubwa ya wananchi waishio vijijini hawafikiwi na elimu za kujikinga na magonjwa ya mlipuko na kufanya magonjwa hayo kusambaa kwa haraka katika jamii zao.

"Tumeona hilo ni tatizo linalotakiwa kufanyiwa kazi kwa karibu zaidi na kazi hiyo sio ya kuiachia serikali pekee lakini na sisi kama wadau wa afya ndio sehemu yetu kuisaidia jamii," alisema.

Baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho walisema hatua hiyo itawasaidia kudhibiti mwenendo wa magonjwa hayo ikiwa ni sehemu ya kujifunza zaidi kwa vitendo.

Ibrahimu Mzarubi, mkazi wa Kata ya Sumve alisema ili kuendelea kudhibiti magonjwa hayo hasa katika kipindi hiki cha mvua serikali ishirikiane na wadau mbalimbali wa afya kutuma wataalamu kuelimisha jamii ili waweze kutumia mbinu na ushauri wa kupambana nayo.


Ukurasa 12

‘Mapishi’ kinamama 2025 yanaporindima waonywa kukwepa rushwa ngono, fedha, kubebwa


Ukurasa 13

**Aambiwa ni mtizamo wa ki-AZAKI si wa wanasiasa wanaotamani dola**


Ukurasa 14

**Juhudi ushirikiano mpya kimkakati kuzuia kasi, ushawishi China, Urusi**



## KARIBU KAMALA HARRIS DAR

# Tanzania na Afrika zitapaa kiuchumi iwapo Amerika itawekeza kwenye nishati

**Na Gaudensia Mngumi**

TANZANIA ni tajiri imejaa kila aina ya rasilimali hata zile za kipekee na zenye thamani na umuhimu mkubwa duniani, mfano uranium au urani ambayo huzalisha nishati safi na salama ya umeme.

Ujio wa Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris ni fursa ya Tanzania kushirikiana na Amerika ambayo inaahidi kuwekeza zaidi Afrika, kama kiongozi huyo anavyonukuliwa akianza safari yake Ghana.

Anakaririwa na wana habari akisema Marekani itaongeza uwekezaji barani Afrika na kusaidia kuchochea kukua uchumi.

Kama hivyo ndivyo, ombi la Tanzania ni kupata utaalamu na teknolojia ili iongezee nyuklia kwenye kapu la nishati au gridi ya taifa.

Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri uzalishaji nishati hasa safi ya maji, aidha gesi, makaa ya mawe na mafuta ni chanzo cha kuchafua anga na kuongeza hewa ukaa, kwa hiyo urani ni moja ya chanzo kinachohitajika sasa kuzalisha nishati salama.

Ni wazi bila umeme wa uhakika uchumi, elimu, afya, kilimo, viwanda na hatima ya Afrika haitafanikiwa. Aidha, uhalifu utakuwa mwingi, mitaa isiyowaka taa usiku si salama, hali kadhalika kazi za hospitalini bila umeme mchana na usiku hazifanyikazi.

Ili Tanzania na Afrika isiwe karakana ya ibilisi Amerika isaidie kupata teknolojia ya umeme salama wa nyuklia, utakaotokana na urani inayopatikana kwa wingi Tanzania na hata Niger.

Dokta Kamugisha Byabato mtaalamu wa uhandisi madini na nishati jadidifu (mining engineering and renewable energy), anashauri kwa namna yoyote ile kuanzisha mradi wa umeme wa nyuklia kwa sababu nishati hiyo ndiyo ufunguo wa maendeleo.


Kamala Harris .**PICHA:MTANDAO.**

Ujio wa Makamu Harris, uwe mwanzo wa kuandaa mipango na mikakati ya kupata nishati salama kwa kuwa ndicho dunia inachohitaji sasa. Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri mataifa yote, bila kujali ni Afrika au Amerika.

Dokta Byabato, anasisitiza kuwa maendeleo ya Ulaya, Marekani na Japan, yamefanikishwa na nishati ya nyuklia tangu miaka ya 1960 na sasa ni zama za kusaidia Afrika kupata nishati hiyo kwenye kapu la umeme kwa vile hakuna anayelenga kurutubisha nyuklia kuzalisha silaha za maangamizi.

Anataja kampuni ya Ufaransa ya AREVA inayochimba urani nchini Niger Afrika Magharibi na uzalishaji wa nishati ya nyuklia, akishauri madini hayo yaisaidie Afrika kuinua uchumi wake kwa vile ikiinuka itasaidia pia kuzalisha bidhaa kama chakula na kupunguza uhaba wa vitu duniani.

“Ni kweli urani inazalisha nishati salama, japo ni madini yenye mionzi mikali na hatari. Kikubwa ni utaalamu na teknolojia ya usalama kwa kila hatua, ili kuepusha athari za mionzi (radioactive materials). Utaalamu na teknolojia vitazuia kuchafua mazingira yetu na kuleta athari, lakini tujaribu pia tupate nguvu kuzalisha umeme huo.”

Mtaalamu huyo anaeleza kuwa nishati ya nyuklia haiathiri jotoanga wala kuongeza joto duniani kama ilivyo umeme wa visukuku (fossils) wa gesi asilia, mafuta na makaa ya mawe.

Anaongeza kuwa japo kuna changamoto kwenye kutunza mabaki ya nyuklia, nchi za Magharibi zinafanya utafiti wa utunzaji wa uchafu utokanao na uzalishaji wa nishati ya nyuklia na kwamba mabaki yote yanatunzwa kwenye matunzo yaliyoandaliwa, hivyo Tanzania na Afrika washirikiane na mataifa yaliyoendelea kupata ufumbuzi wa kuhifadhi taka urani.

Kamishna mstaafu wa Madini , Dk. Peter Kafumu, akizungumzia uwepo wa urani na kama inaweza kutumiwa kuzalisha umeme, anasema inawezekana kwa kutumia utaalamu ili kuepusha athari za mionzi hatari (radio active material).

Anasema urani ipo kwa wingi nchini na sehemu zilipoanza kuchimbwa ni chache ikilinganishwa na kiasi kikubwa ambacho hakijaguswa, mfano inachimbwa Bahi mkoani Dodoma, Manyoni Singida na machimbo ya Mto Mkuju katika wilaya ya Namtumbo mkoa wa Ruvuma.

Tanzania ni tajiri wa urani ipo maeneo mengi kama Mbeya, Njombe, Monduli Arusha, ukanda wa Tabora na Kigoma lakini pia Gallapo mkoani Manyara, anataja mtaalamu huyo mbobezi wa elimu ya miamba -jiolojia, Kuanzia 2024, Tanzania inategemea kuzalisha megawati 2,115 za umeme wa maji kwenye bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, lakini mabadiliko ya tabianchi yanaweza kuikwamisha ndiyo maana kuna umuhimu wa kuchanganya nyuklia kwenye kapu

INAENDELEA UK.12

# ‘Mapishi’ kinamama 2025 yanaporindima watakiwa kukwepa rushwa ya ngono, fedha, kubebwa

## •Wanawake walipuka wapo waliokataa Sh. milioni 100

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

HAWAKUKOSEA wahenga waliosema ‘nguo ya Ijumaa hufuliwa Alhamis’ wakimaanisha matayarisho ya jambo lazima kufanyika mapema.

Msemo huo wa wahenga unaakisiwa na taasisi za kutetea haki za wanawake, kwa kuwaandaa mapema watiania watakaogombea uongozi kwenye uchaguzi mkuu 2025.

Miongoni mwa taasisi wadau za Zanzibar kama Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) Jumuiya za Wanasheria Wanawake (ZAFELA) na ile ya Wanawake Wenyeulemavu (JUWAUZA).

Taasisi hizo zimeanza kuwapa elimu ya uongozi wanawake takribani 100 ikiwaandaa miaka miwili kabla ya uchaguzi mkuu wa 2025 ili kuongeza ushawishi na ushiriki wa kinamama majimboni na idadi ya wanawake ndani ya vyombo vya kutunga sheria.

Wanaonolewa ni kutoka vyama mbalimbali vya siasa vilivyosajiliwa ili ifikapo mwaka 2025 kuvishinda vikwazo vinavyoweza kujitokeza wakisaka nafasi za uongozi wa kisiasa.




Yumna Mmanga akipokea cheti cha ushiriki wa mafunzo ya uongozi yaliyoandaliwa na taasisi za wanawake: **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**WANACHOFUNZWA**

Rushwa ni miongoni mwa wanayofunzwa ,Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) Mwanaidi Suleiman Ali, anasisitiza :”Msikubali kushawishika kwa kupokea hongo zinazotolewa na wanaume ili kuwaachia nafasi.”

Anasema uzoefu unaonyesha kuwa wakati wa uchaguzi huo, wanawake majasiri hukabiliwa na nguvu kubwa ya wanaume wenye fedha nyingi kuwarubuni ili wajitoe na kuwaachia wanapoona wapinzani hao wanakubalika na ni tishio kwao.

Aidha, anaeleza kuwa wapo wanaume wagombea hutumia makundi ya vijana wakiwamo pia wanawake kuwapa mlungula au rushwa, fedha na zawadi kuwaondoa kijanja.

Hata hivyo, kwa upande mwingine anawaomba wanawake waamke na kukataa rushwa ya ngono wanapodaiwa na wanaume wenye maamuzi katika vikao vya kupitisha majina ya wagombea wa nafasi za uongozi katika vyama vyao.

Mwanaidi, anasema ni vyema wanapoona dalili za vishawishi kama hivyo wavikatae mapema na kuripoti ZAECA ili kuwawekea mtego wanaohusika na rushwa zote ikiwamo ya ngono kwa ahadi ya kupitishwa majina yao.

“Ukitakiwa rushwa ya ngono, tumia akili ukusanye ushahidi baadae ripoti ZAECA. Iwapo utajirahisisha kwa tamaa ya kupata uteuzi na kama hukupewa ndio uje ulalamike kwetu, hatutakuwa na namna ya kukupigania maana tunachunguza mchakato mzima ikiwamo mawasiliano ya simu,” anabainisha.

“Umefika wakati wanawake wabadilike na kukwepa mitego ya wanaume wenye uchu, kwani uongozi na cheo hupangwa na Mungu, si kujidhalilisha bali ujasiri na kupambania haki yao.” Anawaambia.

“Kwa mujibu wa sensa ya Tanzania mwaka jana wanawake tupo asilimia 51.Ni jeshi kubwa na tunaweza kuongoza na kushika nafasi za maamuzi kwa njia za haki bila kushusha utu na heshima yetu.,” anasisitiza Mwanaidi.

Baadhi ya washiriki wa warsha hiyo walikiri kuwepo ugumu katika kupata nafasi za kugombea, wingine wakidai mfumo dume ni tatizo hata ndani ya vyama vyao.

Amina Rashid Salum, kutoka Chama cha Wananchi CUF Zanzibar, akizungumzia kuhusu rushwa, anashukuru ZAECA kuwaonyesha njia ya kupata haki, ingawa kuna wasiwasi wa kuwepo muhali hasa kadhia hizo zinapowahusu wenye madaraka.

Amina katika uchaguzi wa 2020 aligombea uwakilishi jimbo la Shaurimoyo, lakini hakupata nafasi, anasema vigogo wanaotuhumiwa na rushwa hakuna hatua zinazochukuliwa hata wanaposhikwa na ushahidi.

Aidha, anaitaka ZAECA kuingia hadi ndani ya chaguzi za vyama vya siasa ambako anadai rushwa imeota mizizi na hata wanapotaja ushahidi, kesi hizo hufumbiwa macho.

Anaeleza uzoefu wa rushwa kuwa wakati akigombea nafasi hiyo mpizani wake mmoja alimfuata kwa kutaka kumrubuni akiahidi kumpatia Shilingi milioni 100, alizozikataa.

“Baada ya kuniona ni tishio alitaka kunirubuni nikamwambia sirubuniwi kwa fedha wala zawadi kama doti za kanga na sabuni”anasema Amina.

Mratibu wa kuwawezesha wanawake katika uongozi (SWIL) unaofanikishwa na Norway, Mariam Ame Chum, anasema lengo lao ni kuwaamsha na kuwaandaa kimbinu wanawake wenye nia ya kugombea uwakilishi, ubunge na udiwani mwaka 2025 ili kuweka mazingira wezeshi ya kufikia 50/50 katika uongozi.

“SWIL imeandaa mafunzo haya ili kuwajengea uwezo wanawake na kuwaondoa hofu ili wajitambue, na tunatarajia wakati ukifika watakuwa wameiva sawasawa,” anasema kutoka TAMWA.

Anasema kutokana na jitihada za TAMWA inayosimama utetezi wa haki za wanawake, hali katika vyombo vya maamuzi imeanza kubadilika, tofauti na ilivyokuwa miongo kadhaa iliyopita wakati Tanzania ikianza mfumo wa vyama vingi.

Mariam pia aliwataka wanaume kuachana na mitazamo hasi kwamba pahala pa mwanamke ni jikoni pekee, akisema katika dunia ya sayansi na teknolojia, wamejitokeza wanawake wingi wanaofanya makubwa kwa maslahi ya mataifa yao.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Salim Suleiman Ali, anawataka wanawake wenye nia ya kugombea uongozi kutengeneza mazingira sasa ikiwa hasa kufanyakazi kwa karibu na jamii.

Anasema, maandalizi hutakiwa kuanza mapema, ili kujua mipango, mikakati, njia za kupita ili kuwafikia wapigakura.

Anasema haiwezekani mwanamke mgombea kutojishirikisha vyema ndani ya chama chake na kugonjea miezi miwili, kabla ya uchaguzi mkuu ndio ajitokeze.

Anazungumzia rushwa ya ngono au fedha akisema ni jambo mojawapo la kukwepa kwa mgombea wanamke, kwasababu humshushia heshima ndani ya chama na jamii.

**WENYEULEMAVU**

Wanawake wenye mahitaji maalumu hawakuachwa nyuma katika kuandaliwa kwa ajili ya kugombea nafasi za uongozi, JUWAUZA ikiwapa kipaumbele.

Yumna Manga ni miongoni mwa wanawake wenyeulemavu anasema ili kuimarisha hali za watu wenye ulemavu lazima kuwepo na ushiriki wa kutosha kwenye vyombo vya maamuzi hasa vya kutunga sera na sheria.

Aidha, anasema uwezo wa kifedha ni changamoto kwa wanawake wenyeulemavu kwenye ushiriki wa siasa kwa sababu kampeni zinahitaji gharama.

“Watu wenyeulemavu tumeachwa nyuma mara tatu zaidi ya mtu mwingine asiye na mahitaji maalumu wengi wetu tunachangamoto ya fedha hivyo tunatoa wito kwa wananchi watuamini kiuwezo ni sio hali zetu”anasema.

Yumna anasema katika uchaguzi wa mwaka 2020 aligombea ubunge viti maalum hivyo amejifunza vitu vingi ikiwamo jamii, inahitaji uelewa wa masuala ya watu wenye ulemavu kwa sababu inamuhukumu kutokana na hali yake na si uwezo wake.

“Hatutaki tu kupata nafasi ya viti maalum tunataka majimbo kuongoza wananchi watuamini tunahitaji kuyasemea mahitaji yetu sisi ndio pilipili inatuwasha”anakumbusha,

Mkurugenzi wa asasi za kiraia -AZAKI Zanzibar Ahmed Abdallah anazipongeza jumuiya za asasi za kiraia kwa elimu wanayotoa kwa wanawake kuhusu nafasi za uongozi ili kuhakikisha wenye ulemavu wanakuwa

## Tanzania na Afrika zitapaa kiuchumi iwapo Amerika itawekeza kwenye nishati

**INATOKA UK.11**

la taifa la nishati.

Amerika ni mfalme wa nishati hasa jadidifu (renewable) na Tanzania pamoja na Afrika ina utajiri wa jua, hivyo juhudi za uwekezaji wa Amerika na Afrika zilenge sekta ya nishati ya jua.

Majiji ya Dar, Mwanza, Dodoma, Arusha, Mbeya na Tanga yanayotarajiwa kuwa makuu na makubwa (megacities), yataimarika kwa kila hali iwapo yataunganishwa na umemejua.

Majengo makubwa, hospitali za kitaifa, rufani na kanda kama Muhimbili, Bugando, Aga Khan, Regence, Dodoma, Benjamin Mkapa lakini pia vyuo vikuu vyote kama UDSM, UDOM, Mkwawa, SUA, Tumaini pamoja na magereza , kambi za majeshi, wizara na hata vituo vya mabasi viunganishwe na umeme jua.

Ifike wakati taa zote za mitaa mijini zijipatie umeme jua kwa vile Tanzania na Afrika zimebarikiwa na jua jingi, karibu kila mkoa una saa takribani 10 za jua kali kila siku achilia mbali upepo ambao ni sehemu ya nishati jadidifu inayopatikana kwa wingi nchini.

Karibu Makamu wa Rais Kamala Harris, Afrika inaposhukuru nchi yako kwa misaada kuanzia ya kiafya kama dawa, kilimo, ufugaji, ujenzi wa miundombinu kupitia taasisi kama USAID, PEPFAR na Millennium Challenge Corporation , ni vyema Marekani irefushe mkono wake na kuisaidia sekta ya nishati ili Afrika isibaki gizani ambako ni karakana ya shetani.

OLENGURUMWA URAIS 2025

# Aambiwa ni mtizamo wa ki-AZAKI si wa wanasiasa wanaotamani dola

•Atetewa ana haki ya maoni yake, wengine ni kampeni, anatumiwa



Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

MWAKA ujao ni wa uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, kisha utafuata mwingine 2025 wa urais, wabunge na madiwani, hivyo ndani ya miaka miwili mfululizo, Watanzania watakuwa wanachagua viongozi kwa mujibu wa katiba.

Wakati huu wa kuelekea katika uchaguzi huo, kumekuwapo na maoni tofauti yanayotolewa na wadau wa siasa yakiwamo ya kuvitaka vyama vya upinzani kumwachia Rais Samia Suluhu Hassan uongozi uchaguzi wa mwaka 2025, wanasiasa wengine wajipange kwa kazi 2030.

Vinashauriwa kuwaweka wagombea wa serikali za mitaa na madiwani na ubunge lakini katika uchaguzi mkuu wamwachie Rais Samia amalizie muhula wa pili.

Ni Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, anayetoa ushauri huo, akieleza sababu zake kuwa ni kutamani kuona nafasi ya urais ikiwaniwa na Rais Samia.

### MARIDHIANO SI KUACHIANA

Kutokana na ushauri wa mwanaharakati huyo, Nipashe imekutana na baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzaani na wachambuzi wa siasa na kuzungumzia suala hilo ili kupata mtazamo wa ushauri wake.

Inaanza na Makamu Mwenyekiti wa ACT -Wazalendo Bara, Dorothy Semu, anayesema, mawazo ya mratibu huyo ni ya ki Asasi za Kiraia (AZAKI) na kwamba wao ni chama cha siasa na lengo lao ni kushika dola si kufanya siasa za vyama visivyo vya kiserikali.

"Tumemsikia Olengurumwa, tunajua mawazo yake, yeye ni mtu wa AZAKI, amekuja na fikra za ki-AZAKI, lakini lengo letu ni kushika dola, tutaweka wagombea katika ngazi zote bila kujali nini kimetokea, yale ni mawazo yake, lakini kama chama cha siasa tutaendelea na harakati zetu, tukiwa na mawazo kama yake, tutaelekea kuwa taasisi za kiraia," anasema Dorothy.

Anafafanua kuwa nia njema aliyoonyesha Rais, ni muhimu kwa kuwa ndiye kiongozi wa nchi, na kwamba hawaendi kwenye maridhiano ili kuachiana nafasi bali kuweka mambo sawa, kwa ajili ya manufaa na mustakabali wa taifa.

Anaongeza kuwa Rais kukutana na vyama ni sehemu ya majukumu yake kama kiongozi wa nchi, ili kuiponya na majeraha, kuweka njia bora ya kulisaidia kusonga mbele, na kwamba hatua hiyo si kigezo cha kuachiana nafasi.

"Chama ambacho hakiko tayari kushika dola, ni chama chenye mawazo ya ki-AZAKI, si ACT- Wazalendo kwa vile tuna malengo hasa kukamata madaraka, yaani mamlaka kamili ya nchi, hivyo si rahisi kuachiana nafasi." Anasisitiza Dorothy.

### KATIBA INARUHUSU

Mchambuzi wa siasa, Gwandumi Mwakatobe, anasema jambo la kwanza kuzingatia ni kuheshimu maoni ya mtu kwa kuwa katiba ya Tanzania inaruhusu uhuru wa kutoa maoni.

"Kwa mantiki hiyo, ninaheshimu maoni yake au mtazamo wake, lakini ni muhimu kutambua kuwa katika suala la uchaguzi, wanaoamua wamchague nani ni wapigakura kwenye karatasi na boksi la kura, hakuna mgombea anayejichagua," anasema Mwakatobe.

Anafafanua kuwa ushauri wa kuwataka wapinzani waache nafasi moja, kwa ajili ya mgombea fulani si sahihi, kwa madai kwamba hajichagui, badala yake waachiwe wananchi au wapigakura waamue wanamtaka nani na lini si kazi ya mtu mmoja.

"Nimeeleza kuwa ninaheshimu maoni na mtazamo wa mtu, kwani katiba imempa raia uhuru wa kufanya hivyo, lakini ni vyema pia tujiulize kama mtu akiachiwa nafasi anaweza kujichagua mwenyewe? Anahoji.

Mchambuzi huyo anasema ushauri wa Olengurumwa unaweza kuzingatiwa, lakini wapigakura wakawa hawautaki au wakaukubali na kwamba waokwenda kupigakura ndiyo wanaotakiwa kuachwa waamue nani wanamtaka awaongoze.

"Niseme tu kwamba, kila mtu ana haki ya kutoa maoni, lakini si lazima maoni hayo yakubaliwe au kukataliwa, ila mkazo wangu ni kwamba, mwenye uamuzi wa mwisho amchague nani ni Mtanzania atakayeweka kura ya ndiyo au hapana wakati ukifika," anasema.

### AU KAMPENI MAALUM

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anasema huenda baadhi ya wapinzani wamepitia kwa Olengurumwa kufanya kampeni baada ya kuona mambo makubwa ambayo amewafanyia kama njia ya kurudisha shukrani na heshima kwa Rais Samia.

"Unakumbuka miaka kadhaa iliyopita vyama vya upinzani vilikuwa na wakati mgumu hadi vikakosa madiwani na wabunge vikasahaulika. Chini ya Mama vimeibuka upya, hivyo si vibaya kurudisha shukrani," anasema Ngawaiya.

Anaongeza kuwa pamoja na hayo, lakini dhana ya vyama vingi, ni kuwa na mtu mwenye uwezo zaidi wa kuongoza bila kujali chama anachotoka, kwa kuwa anayeshinda anakuwa kiongozi wa nchi si wa chama.

"Hivyo inaonyesha Mama Samia ameonekana ni bora zaidi katika nafasi hiyo, ndiyo maana zimeanza kampeni kama hizo, na kama wapinzani wenyewe wamo kwa mlango wa nyuma ni wazi wameona nuru kwa Mama Samia,"anasema.

### WAPINZANI JIBUNI

Aidha, Ngawaiya anawashauri wapinzani kujitokeza hadharani kujadili maoni ya Olengurumwa, ili Watanzania wajue msimamo wao kama wanaungana na mwanaharakati huyo au wanapingana.

"Lakini kwa hali ilivyo ni wazi wameshaona Mama Samia ni bora zaidi. Ninashauri hata katika udiwani na ubunge, wachaguliwe wagombea bora bila kujali vyama wanavyotoka, kwani lengo ni kujenga Tanzania,"anasema.

Olengurumwa, anatoa ushauri huo akisema kutokana na Rais Samia kuonyesha nia ya maridhiano na upinzani, huku vyama vya siasa vikianza kurejea kazini baada ya kuwekwa rumande kwa miaka saba ni vyema kumwachia.

Anasema ni vyema ili kukuza utawala bora na kuongeza utekelezaji wa yale yaliyofikiwa na kuazimiwa.

Mratibu huyo anashauri vyama viweke kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na kwa uchaguzi wa mwaka 2025, wasimamishe madiwani na wabunge na kuachana na nafasi ya urais.

Akikaririwa na vyombo vya habari anashauri vyama vya upinzani kutosimamisha wagombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, akiwa na sababu kadhaa.

Anasema kutokana na Rais Samia kuonyesha nia ya majadiliano na upinzani, huku vyama vya siasa vikianza kurejea tangu kufungiwa shughuli zao kwa takribani miaka saba, ni vyema vikaacha nafasi hiyo, ili kukuza utawala bora.

Mratibu huyo anashauri vyama viwekeze kwa ajili ya uchaguzi unaokuja wa serikali za mitaa , madiwani na ubunge, lakini nafasi ya urais waiache.

Olengurumwa anashauri wafanye hivyo ili angalau wapate theluthi ya wabunge, ya madiwani na wenyeviti wa vijiji kwa uchaguzi unaokuja wa mitaa na mkuu 2025.

"Uchaguzi wa mwaka 2030 waweke wagombea urais, lakini wa 2025 ukiwa wa haki, wapinzani watapata viti vya ubunge, udiwani, hivyo waingie makubaliano na Rais katika uchaguzi huru na haki,"anasema Olengurumwa.

Anafafanua kuwa ili kuwa mgombea urais unahitaji pesa, na akidai wapinzani wana tatizo hilo na kuwataka wawekeze kwa wagombea udiwani na ubunge, huku akiongeza kuwa kwa mtazamo Rais aliyeko madarakani anatekeleza misingi ya wapinzani ikiwamo kuruhusu shughuli za kisiasa.

KAMALA HARISS AFRIKA

# Juhudi ushirikiano mpya kimkakati kuzuia kasi, ushawishi China, Urusi

•Waafrika wajipange ni fursa kuleta yao mezani

NA GAUDENSIA MNGUMI

Ni mwanamama wa kwanza mweusi katika Bunge la Seneti ya Marekani kutoka katika jimbo la California. Mwaka 2017, Kamala Harris, anaapishwa katika bunge hilo.

Katika hotuba yake ya mwanzo, anazungumza kuwatetea wahamiaji na wakimbizi, akiashiria uongozi wa kusimama na wanyonge wa taifa kubwa lenye nguvu, ushawishi kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia duniani.

Akiwa mjumbe wa Kamati ya Seneti ya Usalama na Masuala ya Kiserikali, anapigania ulinzi bora zaidi kwa wahamiaji ambao Marekani huitwa 'dreamers' akitaka uangalizi bora katika vituo vya kuwahifadhi wahamiaji.

Ni kwa mujibu wa andiko lililochapishwa na Mtandao wa Ikulu ya Marekani (White House), yote hayo yanaonyesha kuwa Harris ni mtetezi wa wanyonge, anayetaka haki, maridhiano na kuchukuliana.

Akiwa Seneta, anatetea sheria ya kupambana na njaa, kutoa misaada , kuboresha huduma za afya ya uzazi na kushughulikia athari za mabadiliko ya hali ya hewa kama mjumbe wa Kamati ya Seneti ya Mazingira na Kazi za Umma.

Leo hii Marekani inampa jukumu muhimu katika kuwashirikisha viongozi wa dunia na kuimarisha ushirikiano na ushirika na taifa hilo akilenga mustakabali wa pamoja wa kuwa na Amerika inayosimama na kushirikiana na wengine, unaongeza mtandao huo.

### MBIO URAIS

Makamu Harris, anafikia hatua hiyo, pale anapoanza mbio za kuingia ikulu kupitia chama cha Democrat, anatangaza nia ili kuchuana na bosi wake wa sasa Joseph Biden, akiomba uteuzi wa chama hicho kuwa mgombea kwenye uchaguzi mkuu wa Novemba 2020.

Nyota ya Harris inaanza kung'ara anapoinukia kwa kasi na kujitosa katika kinyang'anyiro cha uteuzi wa urais, wenye msimamo wa kiliberali kwenye chama hicho wakimpenda kwa imani kuwa amebeba mustakabali (hatima na mambo ya baadaye) wa chama chao. Akiwa mwanamama kijana .

Licha ya kuingia katika kinyang'anyiro hicho hakuendelea na mchakato na kumwachia mpinzani wake Joe Biden kupanda na kufanikiwa kwenye mbio za urais.

Wengi walidhani kivumbi hicho kilimmaliza na nafasi yake ya kuwania urais ikawa imepotea, wapo waliodhani kuwa asingekuwa na wadhifa wa makamu wa rais , walikosea, akawa mgombea mwenza 2020 akaanza kazi.

Harris anayekaribia miaka 57 sasa ni binti wa wahamiaji kutoka Jamaica na India. Mwanamama huyu amewahi kuwa mwanasheria mkuu wa jimbo la California ambaye alijulikana na wanaharakati wa kiliberali kutokana na umahiri wa kuuliza maswali magumu kwa wateuliwa wa nyadhifa mbalimbali zinazoidhinishwa na Bunge, wakati wa uongozi wa Rais Donald Trump.

Harris alimgonga maswali magumu Jaji wa Mahakama ya Juu Marekani Brett Kavanaugh na Mwanasheria Mkuu Jeff Sessions, wakati wa vikao vya Seneti vya kuwathibitisha.

Mwaka 2016 baada ya kuweka historia ya mwanamke wa kwanza mweusi kuwa Seneta Marekani kutoka jimbo la California, aliinuka na kuzibwaga sera na wakosoaji wa "siasa za utambulisho", au "identity politics" ambazo anasema zinatumiwa kama dharau ili kuweka kando na haki za watu kwa kuangalia rangi, jinsia na usawa wa kijinsia.

Ni mwanamama mwenye msimamo na mtetezi wa haki, anatajwa na vyombo vya habari kuwa alikuwa miongoni mwa Wanademocrati ambao walimbana na kumhoji Kavanaugh katika kikao chake cha uthibitisho cha kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu kuhusu maoni yake kwenye utoaji mimba na pia kuhusu uchunguzi wa uwezekano wa Urusi kuingilia uchaguzi wa Marekani wa mwaka 2016.

Katika Seneti Bunge la Juu la Marekani, hajaacha kutetea watu wa hali ya chini. Akiwasilisha muswada wa kuzipa familia za kipato cha chini malipo ya pesa taslimu na mikopo kodi ili kusaidia kupambana na hali ngumu ya uchumi na kupanda kwa gharama za maisha kuanzia makazi.

Amekuwa mtetezi mkubwa wa mageuzi ndani ya haki za binadamu hasa suala la haki jinai.

Haki jinai ni kuwatendea haki na kuwaheshimu watuhumiwa wanaofanya jinai kwa kuvunja sheria, kwa kuamini kuwa hata kama wamekosa na wamekiuka sheria wanahesabiwa kama watenda makosa lakini siyo kufanywa waovu, kuteswa, kutopewa haki zao na kutokuthaminiwa utu wao.

### ZIARA AFRIKA

Anapozuru Afrika kwa wiki moja, baadhi ya vyombo vya habari vinasema safari yake inafanyika wakati ambapo Marekani inajaribu kukabiliana na ushawishi wa Urusi na China kwa bara hilo.

Ananukuliwa na AlJazeera, akisema kuwa Marekani itaongeza uwekezaji barani Afrika na kusaidia kuchochea ukuaji wa uchumi , alipoanza ziara yake Ghana.

Ujio wake unalenga kukabiliana na ushawishi wa wapinzani hasa Urusi na China kwa Afrika na kwamba China imewekeza kwa kiasi kikubwa barani Afrika katika miongo ya hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kufanikisha maendeleo ya miundombinu kama barabara, madaraja na rasilimali, wakati ushawishi wa Urusi pia umeongezeka, ikiwa ni pamoja na kusaidia kukomesha uasi kwa kutumwa askari wa kujitegemea wa Jeshi la Wagner Group katika nchi kadhaa zikiwamo za ukanda wa Sahel mfano Mali na Guinea.

"Katika safari yake anakusudia kufanya kazi katika kuongeza uwekezaji barani Afrika na kuwezesha ukuaji wa uchumi na fursa," Harris anasema mara baada ya kuwasili nchini Ghana, taifa la kwanza katika safari ambayo itamfikisha pia Tanzania na Zambia.

"Tunatazamia safari hii kuwa kitu muhimu zaidi katika uhusiano na urafiki wa muda mrefu na wa kudumu kati ya watu wa Marekani na wale wanaoishi katika bara hili," anasema Harris. Katika ripoti ya Al-Jazeera.

Utawala wa Rais Joe Biden, unataka kuimarisha uhusiano na Afrika, ili uwe kama mbadala wa mataifa yanayoshindana, huku kukiwa na ushindani wa kimataifa kuhusu mustakabali wa bara hilo sasa.

"Ni ahadi inayokuja wakati huu kwani zama zilizopita zilionyesha kuwa Marekani ina historia ndefu ya kuingilia masuala ya Afrika, ikidaiwa kuwaunga mkono madikteta dhidi ya vuguvugu la ukombozi na kukwamisha maendeleo kisiasa na kiuchumi, lakini pia ikisukuma kwa bidii kufikia masoko na rasilimali za Afrika na kuacha bara hilo bila chochote," ni maelezo ya Shihab Rattansi wa Al Jazeera. anayekaririwa akiripoti kutoka Washington, DC.

"Kwa hivyo Marekani inasema ni mambo ya zamani sasa, Afrika ni washirika, wote tunaweza kufanikiwa'. Tunachosikia kutoka Afrika ni 'hatutaki kuchagua kati ya China, Russia na Marekani. , lakini tutafanya kile tunachohisi ni kwa manufaa yetu." Inaongeza Al Jazeera.

Kama ya kweli yamekwisha ni zama za kuiona Marekani ikisaidia Afrika kwa kuwa upo ule msemo wa Marshall Plan kuwa kila fedha yake inayokuja Afrika itarudishwa kwa wingi kuliko ile iliyotolewa kama msaada au mkopo.



Kamala Harris. **PICHA: MTANDAO THE WHITE HOUSE**



# Madiwani wawachukulia hatua kinidhamu watumishi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, limewachukulia hatua za kinidhamu watumishi watatu wa halmashauri hiyo huku mmoja akifukuzwa kazi.

Madiwani hao walifikia uamuzi huo juzi katika mkutano wa baraza hilo wa robo ya pili kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 ambao ulipitia na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega, akitoa taarifa ya baraza hilo ambalo lilijigeuza kuwa kamati, alisema kuwa baraza limefanya uamuzi wa kumfukuza kazi Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Maziliga, Elibarick Ombai, kutokana na utovu wa nidhamu.

"Baraza limeamua kutoa adhabu ya juu kwa Mtendaji wa Kijiji cha Maziliga kutokana na tuhuma nzito zinazomkabili na baada ya kukutana na Kamati ya Fedha baraza limeamua kumfukuza kazi mtendaji huyu kwa kushindwa kusimamia majukumu yake," alisema.

**Kuhusu kupunguza hoja za ukaguzi, alisisitiza watendaji hao kupitia kamati ya fedha kushirikiana ili hoja hizo ziwe zimeisha ifikapo robo nyingine mwaka.**

Mkwega alisema mtumishi mwingine ambaye ni aliyekuwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kidarafa ambaye sasa amehamishiwa Kijiji Cha Msiu, baraza limetoa uamuzi wa kumwamuru kurudisha Sh. 601,000 ndani ya miezi mitatu na kupewa onyo kali.

Alisema mtendaji huyo alikusanya fedha hizo badala ya kuzipeleka benki alizitumia kwa matumizi yake binafsi.

Mtumishi wa tatu ni Afisa Elimu vielelezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Nasibu Pangaela ambaye baraza limeamua kumshusha cheo na kuamua abadilishiwe kituo cha kazi wakati akiwa kwenye muda wa matazamio kutokana na kosa la utoro kazini.

Kutokana na hali hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Mkwega aliwataka watendaji wa halmashauri hiyo kutekeleza wajibu wao na kuwasisitiza wakuu wa idara kuweka ratiba za kufanikisha majukumu yao kwa ufanisi.

"Watendaji wangu niwaombe sana mjipange kila mmoja kwa nafasi yake sio lazima tukupe azimio ndio ufanye kazi, tunatamani kuona kila mkuu wa idara anapanga ratiba yake ya kazi ili ilete ufanisi, siku moja baraza hili tuligeuze liwe la kutoa hongera na pongezi kwa watumishi," alisema.

Kuhusu kupunguza hoja za ukaguzi, alisisitiza watendaji hao kupitia kamati ya fedha kushirikiana ili hoja hizo ziwe zimeisha ifikapo robo nyingine mwaka.

"Kwenye kamati yetu ya fedha suala la hoja za ukaguzi tumelitolea muda, yale yanayowezekana kufuta hizo hoja zifutwe kila mmoja kwa nafasi yake hatupendi kuendelea tena kwenye kota inayokuja tukutane na hoja hizo hizo bado zimesimama zilivyo, kila mmoja apambane aone namna anavyoweza kufuta hoja yake," alisisitiza.

# Mama na mwana wapotea kitatanishi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NDUGU wa Theresia Thobias (32) (pichani) waliopo katika mikoa ya Dodoma, Arusha na Kilimanjaro wameungana kumtafuta mwanamke huyo ambaye hajulikani alipo akiwa na mtoto wake George (3) baada ya kupata matatizo ya akili.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili jana, Ruth Thobias ambaye ni dada wa Theresia, alisema mdogo wake alipotea tangu Januari mosi, mwaka huu, akiwa Kibosho Moshi nyumbani kwa baba yake mkubwa.

"Kabla ya kujulikana alipo, alinipigia simu kwa namba ambayo mpaka sasa haipatikani na kuniambia anasafari ya kwenda Tanga, lakini baada ya hapo hajaweza kupatikana tena kwenye simu aliyotumia mpaka sasa alikuwa na matatizo ya afya ya akili maana alikuwa anaongea mambo yasiyoeleweka," alisema Ruth.



Alisema, awali Theresia aliolewa jijini Dodoma, lakini aliachana na mumewe kisha kurejea Arusha kwa wazazi wake ambako huko aliishi kwa muda kabla hajaenda Kibosho kumsalimia baba yake mkubwa.

Ruth alisema huko Kibosho kwa baba yake mkubwa hakuweza kumaliza wiki kabla ya kutoweka kusikojulikana mpaka sasa akiwa na mtoto wake mdogo George.

Alisema pamoja na jitahada za kumtafuta sehemu mbalimbali kwa ndugu, jamaa na marafiki na vituo vya polisi na hospitali, walitoa taarifa Kituo cha Polisi Moshi na kuandikiwa taarifa namba MOS/RB/2466/23.

Ruth alisema pia wanaweza kupiga simu namba 0759 491605, 0719 821447 (Ruth) au 0745 302097 (Veronica), ambaye ni mama yake mzazi.

**Kabla ya kujulikana alipo, alinipigia simu kwa namba ambayo mpaka sasa haipatikani na kuniambia anasafari ya kwenda Tanga, lakini baada ya hapo hajaweza kupatikana tena kwenye simu aliyotumia mpaka sasa alikuwa na matatizo ya afya ya akili maana alikuwa anaongea mambo yasiyoeleweka.**



Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe akipanda mti eneo la mji wa serikali Mtumba, jijini Dodoma juzi, kwenye uzinduzi wa kampeni ya kupanda miti iliyozinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Kumbukeni wenye mahitaji mwezi wa Ramadhani'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKATI waumini ya dini ya Kiislamu duniani wakiwa kwenye mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani wafanyabiashara nchini wametakiwa kutoutumia kwa maslahi yao binafsi ikiwamo kupandisha bei ya bidhaa mbalimbali.

Amewaomba watu wenye uwezo kuwakumbuka waumini wa dini hiyo wasiojiweza wakiwamo wajane na yatima katika kuwasaidia ili wajikwamue kiuchumi kwenye kipindi hiki cha mwenzi mtukufu wa Ramadhani.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Aliwaasa wafanyabiashara wakati wa mwezi huo kuwa ni kipindi cha kumcha Mungu, kuwa na huruma na kushirikiana na sio kukomoana kwa kupandisha bei bidhaa mbalimbali na kuwafanya wasio na uwezo kukosa futari.

"Mwezi mtukufu wa Ramadhani wafanyabiashara wasiutumie wakifikiri ni wa kutoboa kupata zaidi faida na watakaofanya kama ni waumini wa dini ya kiislamu mfungo huo utakuwa ni bure wataonekana ni kama hawajafunga," alisema.

Aliwataka waumini wa kiislamu katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani kuutumia vizuri kwa kushikamana, kutenda mema na kushusha bei, kusaidiana na mafundisho yatakayokuwa yakitolewa ndani ya misikiti yatendwe kwa vitendo vya kumcha Mungu.



# Biashara haramu meno ya tembo yahatarisha utalii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ONGEZEKO kubwa la mauaji ya tembo katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha limeelezwa kuchochewa na biashara haramu ya meno ya ndovu na kuhatarisha idadi ya wanyama hao ambao ni muhimu kwa ustawi wa sekta ya utalii.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki, aliyasema hayo jijini hapo baada ya maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa kushirikiana na maofisa wa Jeshi la Polisi kuwakamata watu watatu wakiwa na vipande 25 vya meno ya tembo.

Ole Meingataki alisema katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari mpaka Machi, mwaka huu yametokea matukio matano ya kukamatwa meno ya tembo vikiwamo vipande 31 pamoja na meno mazima 15.

Alisema pia walibaini mizoga ya tembo katika maeneo mbalimbali ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na yanayoizunguka ikiwa imenyofolewa meno.

"Meno hayo pamoja na vipande hivyo tulipoviunganisha tulibaini kuwa tembo waliouawa ni 22 jambo ambalo ni hatari kwa shughuli zetu za uhifadhi, tembo ni miongoni mwa wanyama muhimu katika hifadhi hiyo kwa shughuli za utalii," alisema Ole Meingataki.

**Machi 25, mwaka huu walifanya msako katika maeneo mbalimbali ya Kata ya Uyole na kuwakamata watu watatu waliokuwa na vipande 25 vya meno ya tembo wakiwa katika harakati za kusafirisha.**

Alisema kwa mujibu wa sheria za uwindaji wa wanyamapori, tembo ni miongoni mwa wanyama wenye thamani kubwa kwenye uhifadhi na thamani yake ni Dola za Kimarekani 15,000.

Alisema kwa idadi hiyo ya tembo waliouawa katika kipindi cha miezi mitatu, serikali imepoteza zaidi ya Dola za Kimarekani 300,000 ambazo ni sawa na zaidi ya Sh. milioni 700.

Alisema mafanikio waliyoyapata ya kukamata meno hayo yametokana na ushirikiano kati ya wahifadhi na Jeshi la Polisi katika mikoa ya Mbeya na Iringa pamoja na wananchi wa maeneo mbalimbali ambao wamekuwa wakitoa taarifa za siri.

Pia alisema katika miaka ya karibuni tatizo la ujangili lilikuwa limepungua kwa kiasi kikubwa, lakini kwa sasa tatizo hilo limeanza kuibuka upya na hivyo kuhitaji nguvu ya ziada kukabiliana nalo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema wamekuwa wakifanya operesheni katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo kwa ajili ya kudhibiti uhalifu na wahalifu.

Alisema Machi 25, mwaka huu walifanya msako katika maeneo mbalimbali ya Kata ya Uyole na kuwakamata watu watatu waliokuwa na vipande 25 vya meno ya tembo wakiwa katika harakati za kusafirisha.

Watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa kwenye moja ya nyumba za kulala wageni katika Kata ya Uyole na walikuwa wameyapanga meno hayo kwenye makasha na kuyaweka kwenye mifuko ya sandarusi.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo na mikoa yote inayozunguka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kuendelea kutoa taarifa za siri wanapowaona majangili ili zisaidie kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria.




Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki, akiwaonyesha waandishi wa habari sehemu ya vipande 25 vya meno ya tembo walivyokamatwa navyo watu watatu katika moja ya nyumba za kulala wageni jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Kuta zenye nyufa zahatarisha maisha ya wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Nyeregete katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wapo hatarini kuangukiwa na kuta za madarasa zenye nyufa kutokana na kutokarabatiwa kwa muda mrefu.

Aidha baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wanalazimika kukaa chini kutokana na shule hiyo kukabiliwa na upungufu wa madawati.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Amina Mwachuma, aliyasema hayo wakati wa kupokea msaada wa madawati 100 kutoka kwa jumuiya ya Nyeregete.

Alisema shule hiyo ina hali mbaya ambayo inahatarisha maisha ya wanafunzi kwa maelezo kuwa baadhi ya madarasa yana nyufa kutokana na shule hiyo kuwa ya siku nyingi.

Aliiomba serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kusaidia kuboresha miundombinu hiyo kabla haijaleta madhara kwa wanafunzi wa shule hiyo.

"Hali ya shule yetu sio nzuri kabisa, kuta zina nyufa na hatari kwa maisha ya watoto wetu, tunaiomba serikali iliangalie hili ili watoto wetu wasome kwenye mazingira mazuri," alisema Mwachuma.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Nyeregete, Tumain Mpande, alisema shule yake ina zaidi ya wanafunzi 600 na kwamba mbali na uchakavu wa majengo pia inakabiliwa na tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo.

Vilevile, ina idadi ndogo ya walimu ambayo inawalazimu waliopo kubeba mzigo mkubwa wa kufundisha masomo mengi bila kupumzika walimu waliopo ni sita pekee.

"Nawashukuru wadau wa shule yetu kwa kuguswa na tatizo hili la madawati, lakini hali si njema kwa watoto wetu, mazingira ya kujifunzia sio rafiki," alisema mwalimu Tumain.

## TBS yatoa mafunzo kwa wajasiriamali usindikaji bidhaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Viwango nchini (TBS) limeanza kutoa mafunzo maalumu kwa wafanyabiashara, wajasiriamali na wasindikaji wa bidhaa mbalimbali ili kuwasaidia kuzalisha bidhaa zenye ubora ambao utakidhi ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa juzi jijini hapo na wadau mbalimbali walishiriki ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Viwango barani Afrika ambayo hufanyika Oktoba 14, kila mwaka.

Akifungua mafunzo hayo juzi, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alilishukuru shirika hilo kwa kuanzisha mafunzo hayo akieleza kuwa yatawasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa ambazo zitakuwa na ubora unaokubalika katika soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema ili kuendelea kuboresha viwango vya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali, TBS inatakiwa kuweka maofisa wake mpaka katika ngazi ya kata ili wananchi wasogezewe zaidi huduma kwenye maeneo yao ya uzalishaji.

Alisema utaratibu huo unaweza ukawa na tija kama ilivyofanya Wizara ya Kilimo kwa kuweka maofisa kilimo katika ngazi hiyo na kuleta matokeo chanya.

Awali, Meneja wa Viwango wa TBS kutoka makao makuu, Mhandisi Yona Afrika alisema mafunzo hayo yalikuwa yanawalenga wasindikaji wa mazao ya kilimo ili wajue umuhimu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Alisema utaratibu huo utawasaidia kuzalisha bidhaa zenye viwango ambavyo vitakuwa na ushindani na zitaaminika na watumiaji kutokana na kuwa na nembo ya ubora.

Alisema kazi ya kuandaa viwango vya bidhaa mbalimbali ni ya wadau wakiwamo wakulima ambao ndio kundi la kwanza kwenye mnyororo wa uzalishaji, lakini kundi hilo lilikuwa linasahaulika.

Meneja wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Abel Mwakasonda, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuendelea kushiriki katika mafunzo mbalimbali ya ubora yanayotolewa ili wazalishe bidhaa zenye ubora.

Alisema mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa kwa wazalishaji kwa sababu yanasaidia kulinda afya za watumiaji wa bidhaa hizo pamoja na kuendana na matakwa ya kisheria.

# Kiwanda kusarifu dagaa chaanza kujengwa Kama

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeanza ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Kama Wilaya ya Magharib A Unguja, ikiwa ni juhudi za kuinua pato la wajasiriamali wadogo.

Wakizugumza jana katika ziara ya kuangalia eneo linalojengwa kiwanda hicho, kamati ya mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na watendaji wa taasisi mbalimbali za serikali walisema kujengwa kwa kiwanda hicho ni kuwasaidia wajasiriamali kutumia njia za kisasa za kuanika na kukausha dagaa.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema serikali ilipanga mpango wa kuwakusanya wafanyabiashara ya dagaa katika maeneo mawili ya kuendeleza biashara ya uanikaji wa dagaa katika maeneo ya Kama na Funguni, Unguja na kwamba kujengwa kwa kiwanda hicho kutawasaidia kufanya harakati zao kwa urahisi kutokana na kuwekewa miundombinu ya kisasa.

**Dhana ya uchumi wa buluu ni kuwasaidia waanika dagaa ili kuendana na ushindani wa masoko ya kimataifa.**

Alisema dhana ya uchumi wa buluu ni kuwasaidia waanika dagaa ili kuendana na ushindani wa masoko ya kimataifa.

Alisema ameridhika na ujenzi katika eneo hilo kwa kuwa lina uwezo wa kuwakusanya wajasiriamali wengi kufanya harakati zao katika eneo moja.

Waziri wa Mawasiliano, Usafirishaji na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema serikali itajenga miundombinu ya kisasa inayohitajika katika eneo hilo kabla ya kuwahamisha wajasiriamali hao katika maeneo yao ya awali.

Alisema kuwahamisha wajasiriamali hao katika sehemu za awali kunatokana na maeneo hayo kufanywa shughuli za uwekezaji ikiwamo ujenzi wa bandari kwa ajili ya makasha ya mizigo na ujenzi wa hoteli.

Mohamed ambaye pia ni Mwenyekiti wa kamati ya mawaziri wanaosimamia mradi wa ujenzi wa mradi huo, alisema licha ya mazingira mazuri katika eneo hilo la kiwanda, lakini kunahitajika maboresho ya uwekaji wa miundombinu ya maji, umeme na vyoo ili kukidhi mahitaji ya wajasiriamali.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Rahma Kassim Ali, alisema eneo hilo litapimwa ili lisivamiwe na wananchi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makaazi.

Aidha, alisema atahakikisha eneo hilo halifanyiwi uharibifu wa mazingira ili kudumu kwa miaka mingi na kuleta manufaa kwa taifa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema atahakikisha anasimamia masuala ya ulinzi na usalama katika eneo hilo ili ulinzi udumu wakati wote katika eneo hilo.

Meneja mradi wa ujenzi wa kituo hicho cha usarifu wa madaga, Pius Nteule, alisema kiwanda hicho kitakapomalizika kitakuwa na uwezo wa kuajiri wajasiriamali 10,000.



Mkuu wa Uhifadhi katika Kisiwa cha Chumbe, Omar Nyange Ame, akitoa maelezo kwa waandishi wa habari jana, kuhusu msikiti wa zamani wa kihistoria uliojengwa mwaka 1096 kisiwani hapo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ: Hatukubali vitendo vya ushoga

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Zanzibar haipo tayari kukubali vitendo vya ushoga na ipo tayari kukosa misaada kutoka kwa mashirika ya kimataifa ambayo inaruhusu vitendo hivyo.

Alisema vitendo vya ushoga ni kinyume na maadili ya utamaduni wa Watanzania, lakini pia ni kinyume na mafundisho ya dini.

Aliyasema hayo mjini hapo mwishoni mwa wiki katika maadhimisho ya siku ya ustawi wa jamii na kuonesha kukerwa na baadhi ya matukio hayo.

"Vitendo vya ushoga ni kinyume na maadili ya utamaduni wetu na kamwe serikali haiwezi kuvumilia vitendo hivyo vichukuwe nafasi katika jamii yetu," alisema.

Aidha, alisema jamii inahitaji kuchukua juhudi za makusudi ikiwamo kukemea vikali aina zote zenye kuonesha matukio ya ushoga ili kuwa na kizazi chenye maadili mema.

"Wapo watu wengine wanasema tukikemea vitendo vya ushoga basi tutakosa misaada inayotolewa na mashirika ya kimataifa kama sharti lao ni hilo tunyamaze ni bora tukose misaada na msitupe hata shilingi, lakini kamwe haturuhusu matukio hayo ambayo ni ya aibu," alisema.

Aidha, alilitaka Jeshi la Polisi kupambana na watu wanaojirusha katika mitandao ya kijamii kwa kuonesha picha zinazokwenda kinyume na maadili ya Mzanzibari.

Alisema kumejitokeza matukio mengi ya wanaume na wanawake kutumia mitandao ya kijamii vibaya kwa kuonesha picha ambazo hazina maadili kitendo kinachotakiwa kudhibitiwa haraka.

Hata hivyo, Hemed alikemea baadhi ya taasisi zinazokusanya misaada kwa watoto yatima kuitumia kwa maslahi yao binafsi huku wakijikusanyia fedha kinyume na malengo.

Alisema jamii inayo dhima kubwa katika kulinda watoto yatima kwa sababu wametajwa katika vitabu vyote vitakatifu katika kuwalinda watoto hao ambao wameondokewa na wazazi wao.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema bado wizara haijaridhishwa na kasi ya kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia katika mahakama mbalimbali za Unguja na Pemba na kuivunja moyo jamii kukata tamaa.

**Jamii inayo dhima kubwa katika kulinda watoto yatima kwa sababu wametajwa katika vitabu vyote vitakatifu katika kuwalinda watoto hao ambao wameondokewa na wazazi wao.**

# Serikali kushughulikia tatizo la ukosefu huduma za kijamii Bumbwini Kiyongwe

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI ya Zanzibar, imeahidi kushughulikia changamoto za wakaazi wa Kijiji cha Bumbwini Kiyongwe za ukosefu baadhi ya huduma muhimu za kijamii zinazowakabili ili kuleta ustawi bora wa maendeleo ya kijamii.

Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, alisema hayo huko Bumbwini Kiyongwe, Wilaya ya Kaskazini B Unguja, akiwa katika mfululizo wa ziara za kuwakagua na kuwafariji wagonjwa na wananchi waliopatwa na misiba katika mkoa huo.

Alisema serikali imepokea kutoka kwa wananchi na kuona kero kubwa ya ukosefu wa usafiri wa barabara jambo linalochangia kudhoofisha shughuli za kimaendeleo kwa wananchi wanaoishi kwenye kijiji hicho.

Othman ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, alisema kero kubwa ya barabara, inachangia wahudumu wa afya na walimu kutofika na kurudi kwa wakati katika vituo vyao vya kazi ndani ya kijiji hicho na kero hiyo serikali itaishughulikia na kuipatia ufumbuzi.

Aidha, Othman aliwataka viongozi wa Chama cha ACT- Wazalendo katika ngazi ya wilaya na mikoa kuiga mfano wa wenzao wa mjini kuanzisha mifuko ya faraja itakayotumika kusaidia kutatua changamoto walizonazo wananchi kwenye maeneo yao.

Wakazi wa kijiji hicho walisema hawana barabara kwa muda mrefu jambo linalochangia wananchi kupata shida ya kuingia na kutoka katika kutekeleza shughuli zao za kimaendeleo huku wahudumu wa afya na walimu wa shule ikidhoofisha utekelezaji wa majukumu yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**GODFREY MSOFE** anatangaza kupotelewa na cheti cha Degree of Bachelor of Education chenye namba **TU/M/Bed/09/1110** kilichotolewa na **TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA** mwaka 2012. Cheti cha Masters of Education in Curriculum and Instructions chenye namba **T/MAS/2018/0032** kilichotolewa na **MWENGE CATHOLIC UNIVERSITY** mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **ARU/ARU/RB/109246/2023 na ARU/ARU/RB/109249/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**GODFREY MSOFE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0376-0007** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SONI SEMINARY** mwaka 1999. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0164-0510** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **USA SEMINARY** mwaka 2002. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **ARU/ARU/RB/109244/2023 na ARU/ARU/RB/109245/2023.**

## REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT
(CAP 117)

### DEED POLL

**BY THIS DEED, I TOFA SALEH SULEIMAN,** an Adult Muslim of Dar es salaam, do hereby renounce the name of **TOFA WAHID JUMA** as my name, and in lieu thereof do assume and adopt the name of TOFA **SALEH SULEIMAN** as it appears in my National Identity Card No. **19610624-11466-00001-15** respectively.

**AND IN PURSUANCE** of such change of name as aforesaid, **I DO HEREBY DECLARE THAT,** I shall at all times hereafter in all records, deed and instruments in writing and in all actions, proceedings, and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever, use and sign the said name of **TOFA SALEH SULEIMAN** as aforesaid. **AND I HEREBY AUTHORISE** and request all persons and authorities to designate and address me, in the name of **TOFA SALEHE SULEIMAN only.**

**IN WITNESS WHEREOF** I have hereunto subscribed my name of **TOFA SALEH SULEIMAN,** on the date and manner hereunder appearing:

**SIGNED and DELIVERED** by the said TOFA **SALEHE SULEIMAN** who is personally know to Me, in my presence on this 15th Day of the Month of April, in the year of our Lord 2021.



TOFA SALEH SULEIMAN
DEPONENT

BEFORE ME: HAIDER TWAHIR MWINYIMVUA
Signature:
Postal Address: P. O. Box 106228, DAR ES SALAAM
Qualification: ADVOCATE/COMMISSIONER FOR OATHS & NOTARY PUBLIC

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**INNOCENT JOSEPH MASSAWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T798CAZ** aina ya Suzuki **ESCUDO,** Chassis No.**TL52W100195,** Engine No. **ILFE2431.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/111420/2023**

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA BAJAJ

**DICKSON MATHIAS MLELWA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya BAJAJ yenye namba za usajili MC 648 CGE. Chassis Namba: MD2A25BYOKWM27901. Engine Namba: AZZWKM36530.

Kadi Namba: 8117712. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/111708/2023.**

## NOTISI/ TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kwa mamlaka tuliyopewa na **VICTORIA FINANCE PLC, AKIBA COMMERCIAL BANK PLC , BRAC na NMB BANK** kwa mujibu wa sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,tunatoa notisi ya kulipa madeni kwenye taasisi zote nne kwa mdaiwa hapo chini ndani ya siku 7 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa marudio wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| s/No. | Jina la Mdaiwa | Jina la mdhamini | Dhamana | Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | Nyumba | KIMARA TEMBONI MTAA WA MJIMPYA-UBUNGO | 06/04/2023 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0788411524/0714939933.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**VERONICA JOHN UFUNGUO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 347 BQX – BENZ.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 244 CNZ – GRAND HIACE.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/112204/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZNIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha KIHONDA**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 13/2023**
**Jina la Mdai: JALUO NASSA MTEMI**
**Jina la mdaiwa: SANDRA CHRISTINA BODMARK**

## KUITWASHAURINI

(Kanuni ya 18 ya kanuni ya taratibu za madai katika mahakama za mwanzo)

**Kwa: SANDRA CHRISTINA BODMARK**


Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za mdai)

**TALAKA**

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 30 mwezi wa 03 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mijibu wa madai hayo vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitikwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mhakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri ns Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 24 mwezi 03 mwaka 2023




## LOSS OF CERTIFICATE OF REGISTRATION

Ndugu **Albert Juliano Simwanza** anatangaza kupotelewa na cheti cha usajili chenye namba za usajili **SO.NO.5201** (Kanisa la Neema Tanzania).

Kwa yeyote atakayekiona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/111947/2023**

## KUPOTEA KWA HATI

Mimi **ZUBERI YANGAYA BAKARI** natangaza kupotelewa na hati ya nyumba,

**Plot Na. 68 Block "A"** Makorora – Tanga Mjini.

Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi

Taarifa ya Polisi: **TAN/RB/514202/2021**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Mwananchi aliyekutwa na kamera jirani na eneo ambalo lilikuwa linachomwa moto matairi, kutokana na vurugu za baadhi ya waandamanaji nchini Kenya. Mamlaka Huru ya Kusimamia Polisi nchini Kenya (Ipoa), imesema inachunguza matukio mawili ya siku ya juzi. **PICHA: BBC**

## VURUGU KENYA;

# Odinga alaani uvamizi na uharibifu mali za Kenyatta

## ...AU yatoa angalizo

**Nairobi, KENYA**

KIONGOZI wa muungano wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga amelaani uvamizi wa mali ya aliyekuwa rais wa taifa hilo, Uhuru Kenyatta.

Polisi nchini humo walitembelea shamba linalomilikiwa na familia ya Kenyatta, baada ya sehemu ya shamba hilo kuteketezwa na wavamizi siku ya Jumatatu.

Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AU), Moussa Faki Mahamat, alionesha wasiwasi wake kuhusu ghasia zilizotokea na kusababisha kifo cha mtu mmoja, huku mali ya thamani isiyojulikana ikiharibiwa baada ya maandamano dhidi ya serikali.

Katika taarifa iliyotiwa saini na Umoja huo, mwenyekiti huyo, sasa alitaka washikadau kuweka utulivu na kuanzisha mazungumzo, ili kuangazia tofauti zilizopo, kwa lengo la kuleta umoja na maridhiano.

Aidha, aliwakumbusha Wakenya kuhusu ufanisi wa uchaguzi wa Agosti, mwaka jana, nchini humo na uthibitisho uliofuatia wa matokeo ya uchaguzi na Mahakama ya Juu.

Juzi, wavamizi walikata miti na kuchukua kondoo kutoka katika shamba hilo lililo pembezoni mwa mji mkuu, Nairobi.

Maofisa wa polisi waliokuwa na silaha walikuwapo na hawakuingilia kati, kulingana na ripoti za ndani.

Siku ya jana, maofisa wa polisi walitembelea shamba hilo na kutathmini uharibifu lakini wamekosolewa kwenye mitandao ya kijamii kwa kuchelewa sana kuchukua hatua.

Polisi bado hawajatoa tamko kuhusu uvamizi huo.

Katika mahojiano kiongozi huyo wa upinzani, Odinga, alisema alidai anaamini shambulio hilo lilitekelezwa na 'majangili' waliokodishwa na serikali.

Kenyatta ni mshirika wa Odinga. Jumatatu, wiki hii, ilikuwa siku ya pili ya maandamano dhidi ya serikali yaliyoitishwa na Odinga kwa madai kwamba, kulikuwa na udanganyifu katika uchaguzi uliopita pamoja na kupanda kwa gharama za maisha.

Kuporwa kwa shamba kubwa la Kenyatta na wavamizi, kunaonekana kama kulipiza kisasi kwa hatua yake ya kumuunga mkono, Odinga.

Maandamano zaidi yanapangwa, siku ya Alhamisi wiki hii. Lakini serikali imelaani ghasia na usumbufu unaosababishwa na maandamano hayo.

Odinga aliiambia BBC kuwa hajahusika na uharibifu wa mali akidai waandamanaji wanatetea haki ya kikatiba ya kuandamana.

Alisema ni bahati mbaya kwamba waandishi wa habari walilengwa na polisi na waandamanaji wakati wa maandamano ya Jumatatu.

Baadhi ya watu walionekana wakitoka shambani wakiwa wamebeba kondoo mabegani mwao.

Odinga, alikosoa baadhi ya sera za kiuchumi za Rais William Ruto, akisema ingawa gharama ya maisha ni tatizo la duniani kote, nchi nyingi zimejaribu kuwaokoa raia wao kutokana na mdororo wa kiuchumi, akidai Ruto ameondoa ruzuku na wananchi na wanateseka zaidi sasa.

Alisema yuko tayari kukutana na Rais Ruto kwa mazungumzo, lakini akataja masharti mawili yanayohitaji kuafikiwa.

Kwanza, akisema sera za uchaguzi za kielektroniki zifunguliwe, ili kuthibitisha ikiwa kura ya mwaka jana iliibiwa na pili, uteuzi wa makamishna wapya wa tume ya uchaguzi unapaswa kuhusisha pande zote.

Mahakama ya Upeo ya Kenya, ilitupilia mbali kesi ya Odinga kupinga kushindwa kwake katika uchaguzi wa Agosti mwaka jana, lakini bado anasisitiza kuwa uamuzi huo uliathiriwa.

Uvamizi huo unatokea ikiwa ni wiki ya pili ya maandamano dhidi ya serikali na kutokea visa viwili vya uharibifu wa mali, zinazohusishwa na Odinga na rais wa zamani, Kenyatta.

Watu wasiojulikana walivamia kampuni ya East Africa Spectre Limited katika barabara ya Mombasa na kuharibu mali.

Kampuni hiyo ni ya utengenezaji na usambazaji wa mitungi ya gesi inahusishwa na familia ya Odinga.

Meneja wa Ulinzi na Usalama katika kampuni hiyo, Humphrey Waswa aliviambia vyombo vya habari kuwa, takriban watu 50 walifika kwenye eneo hilo wakiwa kwenye pikipiki mwendo wa saa tano asubuhi na kuwashambulia.

"Walikuwa wakisaidiwa na magari manne ambayo hayakuwa na nambari za usajili, Land Cruiser na tunashuku kuwa lengo lao, lilikuwa ni mkurugenzi wetu mkuu kwa sababu ofisi yake ndiyo imeharibika sana," alisema.

Waswa alisema kampuni itatoa taarifa za kina baadaye baada ya uchunguzi kufanyika na kuhitimishwa.

Hakuna aliyejeruhiwa wakati wa tukio hilo.

Kampuni ya maziwa ya Brookside Dairy na shule ya Peponi, zipo ndani ya ardhi hiyo. Hakuna tamko lililotolewa na polisi kuhusu matukio yote mawili.

*BBC*

# Shujaa 'Hotel Rwanda' aenda uarabuni kubarizi

**Doha, QATAR**

PAUL Rusesabagina, ambaye aliigiza kama shujaa katika filamu ya Hollywood Hotel Rwanda, amewasili Doha, nchini Qatar baada ya kuachiliwa huru kutoka gerezani, nchini Rwanda.

Ofisa wa Ikulu ya Marekani, alisema Rusesabagina aliondoka Rwanda juzi na kufika katika mji mkuu wa Qatar, Doha.

"Naweza kuthibitisha kwamba Paul Rusesabagina ameondoka Rwanda na kwa sasa yuko Doha," Mratibu wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Marekani, John Kirby alinukuliwa kwenye ripoti hiyo.

"Hivi karibuni atarejea Marekani. Na familia yake, kwa vile nina hakika hakuna anayeshangaa, wana hamu ya kumkaribisha tena hapa nyumbani."

Mazungumzo yaliyosimamiwa na Qatar yalipelekea kuachiliwa kwake kutoka gerezani mwishoni mwa wiki ikiwa ni miaka miwili baada ya kuhukumiwa miaka 25 gerezani kwa ugaidi.

Wafuasi wake waliita kesi hiyo kuwa ya udanganyifu. Adhabu hiyo ilibadilishwa kwa amri ya rais, kulingana na msemaji wa serikali.

Ilifuata miaka ya shinikizo la kidiplomasia na Marekani, ambako Rusesabagina alikuwa akiishi tangu mwaka 2009.

Rusesabagina anasifiwa kwa kuokoa watu takribani 1,200 wakati wa mauaji ya Kimbari yaliyotokea mwaka 1994 nchini Rwanda.

*BBC*

**"Naweza kuthibitisha kwamba Paul Rusesabagina ameondoka Rwanda na kwa sasa yuko Doha," Mratibu wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Marekani, John Kirby alinukuliwa kwenye ripoti hiyo.**

# SABABU YANGA PRINCESS KUMTIMUA TENA KOCHA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imemtimua Kocha Mkuu wa timu ya soka ya wanawake, Yanga Princess, Sebastin Mkoma, baada ya mwendelezo mbaya kwenye Ligi Kuu inayoendelea.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, imesema imevunja mkataba wa kocha huyo baada ya makubaliano ya pande mbili.

Aidha, taarifa hiyo iliyotolewa na Ofisi ya Mtendaji Mkuu, imesema kuwa kwa sasa benchi la ufundi litakuwa chini ya Kocha Fred Mbuna mpaka msimu huu wa ligi utakapomalizika.

"Uongozi wa Klabu ya Yanga unapenda kuutaarifu umma kuwa umefikia makubaliano ya kuvunja mkataba na Kocha Mkuu wa timu ya Wanawake, Yanga Princess, Sebastian Mkoma.

"Uamuzi huo umefikiwa baada ya makubaliano ya pande zote mbili. Uongozi wa Yanga unamshukuru kocha Sebastian kwa kazi yake kipindi chote alichokuwa akiifundisha timu yetu ya wanawake. Kwa sasa benchi la ufundi la Yanga Princess litakuwa chini ya kocha Fred Mbuna mpaka msimu huu utakapomalizika," ilieleza taarifa hiyo.

Mbuna ambaye zamani alikuwa beki wa kulia wa Majimaji na Yanga, alikuwa akihudumu katika timu hiyo chini ya Mkoma.

Mkoma ametimuliwa baada ya kuhudumu kwa miezi mitatu, akitokea Simba Queens ambapo aliiwezesha timu hiyo kutwaa ubingwa msimu uliopita.

Yanga Princess ilimtwaa kocha huyo baada ya kumtimua aliyekuwa kocha wao, Edna Lema, mwanzoni mwa Desemba mwaka jana.

Timu hiyo imekuwa haipati matokeo mazuri yaliyokusudiwa msimu huu kwani inashika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu ikiwa na pointi 22, pia ikicheza mechi tatu bila ushindi, ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Fountain Gate Princess, na sare ya bao 1-1 dhidi ya vibonde Mkwawa Queens na watani zao wa jadi Simba Queens hivi karibuni.

**TUPO TAYARI...**




Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi ya mwisho jana asubuhi katika Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam kabla ya kukwea pipa kuelekea nchini Morocco tayari kwa mchezo wa kukamilisha hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablanca utakaopigwa Jumamosi wiki hii. **PICHA: SIMBA**

# Naibu Waziri aipongeza NBC kuinua michezo

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Waziri wa Utamaduni, Sanaa, na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, ameipongeza Benki ya NBC kutokana na jitihada zake za kusaidia maendeleo ya michezo mbalimbali nchini.

Mwana FA, aliyasema hayo wakati wa hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi wa mchezo wa gofu wa NBC Lugalo Open 2023, iliyofanyika katika viwanja vya Jeshi Lugalo juzi.

Alisema Benki ya NBC imekuwa ikitoa mchango mkubwa katika sekta ya michezo hapa nchini na kuongeza kuwa serikali inatambua mchango wa benki hiyo.

"Nikiwa Naibu Waziri mwenye dhamana ya Utamaduni, Sanaa, na Michezo, napenda kuishukuru Benki ya NBC kwa kutuunga mkono katika jitihada za kuendeleza na kukuza maendeleo ya michezo nchini," alisema.

"NBC imekuwa ikifadhili michezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara, Dodoma Marathon. Ligi yetu kwa sasa ni moja ya ligi zinazotajwa kuwa ni bora barani Afrika na hii imewezekana kutokana na mchango wa Benki ya NBC," alisema.

Aliongeza: "Ni rai yangu kwa NBC kuendeleza kuweka mkono kwenye michezo yetu na katika sehemu nyingine za kijamii hapa nchini. Makampuni na taasisi nyingine pia ziige wanachokifanya NBC ili tuweze kupiga hatua kubwa na kwa haraka zaidi.

"Sikutegemea kuwakuta kwenye gofu, nimefurahishwa na jitihada zenu kwa kuwa mstari wa mbele katika kukuza na kuimarisha michezo Tanzania. Hongereni sana NBC ninyi ni mfano wa kuigwa".

Aidha, Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa NBC hiyo, James Meitaron, alisema kupitia sera ya kurudisha kwa jamii, benki hiyo itaendelea kuunga mkono jitihada za serikali kuendeleza na kukuza michezo mbalimbali nchini.

"Tunaamini kuwa ushiriki wetu kwenye eneo hili la michezo pamoja na kusaidia juhudi za serikali katika maeneo mengine, utasaidia kuboresha maisha ya Watanzania ikiwa pia ni sehemu yetu ya kurudisha kwa jamii," alisema na kuongeza:

"Kama tulivyoahidi hapo awali, leo tumetoa tuzo mbalimbali kwa washiriki wa mashindano haya ya Wazi ya NBC Lugalo 2023".

Kwa upande wa mshindi wa kwanza wa mashindano hayo, Ally Mcharoh, alishukuru NBC kwa kudhamini na kufanikisha mashindano na pia aliushukuru uongozi wa Klabu ya Gofu ya Lugalo kwa kukubali kufanya mashindano hayo na kuwapa fursa vijana kuweza kuonesha vipaji vyao.

# Meridianbet yaja na Jackpot kedekede

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wateja wao wanaendelea kunufaika kimapato, Kampuni za Mchezo wa Kubashiri ya Meridianbet imekuja na bonasi babkubwa, 'odds' kubwa na Jackpot kedekede kupitia mchezo wa Sloti ya Foxpot kutoka kasino ya mtandaoni ambao utakuwa na magurudumu 12 ya ushindi.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet, Martin Nkurlu, akizungumza na gazeti hili jana, alisema Sloti hii ya Foxpot ina alama na machaguo mbalimbali na kwamba ili ushinde, unatakiwa upate alama tatu zenye kufanana kwenye sloti yenye kolamu tano na mstari mmoja wa malipo.

Alisema ni wewe tu kuchagua lipi unaenda nalo, lakini bila kusahau kabisa kuna chaguo la Mbweha ambaye ni ishara ya malipo ya mawindo yako.

"Kasino ya mtandaoni ya Meridianbet ina machaguo mbalimbali ambayo yanakupa fursa ya wewe mchezaji kuucheza mchezo huu kiurahisi kwa kubofya alama ya + na ambazo zipo kwenye kitufe cha bet, itakupa nafasi ya kuweka dau lako unalolitaka.

"Huenda ukawa sehemu ya washindi wakubwa kila siku kutoka kasino ya mtandaoni ya Meridianbet, pata bonasi kibao na ushindi mkubwa mara 1000 ya dau lako uliloweka kutoka sloti ya Fox-Pot," alisema Nkurlu na kuongeza:

"Ni rahisi sana! Unachotakiwa kufanya ni kuingia kwenye kasino ya mtandaoni ya Meridianbet na kuchagua mchezo huu wa Foxpot ujishindie mamilioni, kuna chaguo la 'Autoplay' ambalo litakuwezesha wewe (mchezaji) kuzungusha mizunguko 'kiautomatiki'," alisema Mkuu huyo wa kitengo cha masoko.

Alisema alama za sloti hii ni ya matunda ambayo ni Cherry, lina thamani ndogo, Zambarau ambalo litakurudishia mara 1.5 ya dau lako huku likifuatiwa na Ndimu ambalo litakulipa mara 2.5 ya dau ulilowekа.

Alisema endapo utapa alama 1, 2 au 3 za Lucky 7, basi utalipwa mara tatu ya dau ulililoweka huku alama moja ya Lucky 7, ikiwa ina uwezo wa kukulipa mara 10 ya dau lako, na alama 2 za Lucky 7 zikitakurudishia mara 15 wakati alama 3, zitakurudishia mara 25 ya dau lako.

Nkurlu alisema ukipata alama ya 'Wild' utarudishiwa mara 40 ya dau lako na kwamba alama hiyo inauwezo wa kubadilisha alama zozote kwenye mchezo huu na kukupatia ushindi isipokuwa alama ya bonasi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY YAKATALIA PHILLIPS

KLABU ya Manchester City haina mpango wa kumuuza kiungo wake wa kati, Kalvin Phillips msimu wa majira ya joto, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kucheza mechi chache tu tangu kuhamia hapo Etihad akitokea Leeds United. ***(Football Insider)***

### KALVIN ATAKA KUONDOKA

HATA hivyo, mwenyewe Kalvin Phillips anasemekana kuwa atakuwa tayari kuondoka Manchester City huku kukiwa na hofu kwamba kukosa muda mwingi wa kucheza kunaweza kuathiri nafasi yake ya kuchaguliwa kwenye kikosi cha England. ***(90MIN)***

### MESSI KWENDA MAREKANI

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, anaweza kuhamia Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS), msimu huu wa majira ya joto. ***(Sport)***

### KANTE ATAKIWA PSG

KLABU ya PSG inaendelea kuwasiliana na wawakilishi wa kiungo wa kati wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31kwa ajili ya kumsajili. ***(90min)***

### RODRIGO KUPUNGUZA MSHAHARA

MSHAMBULIAJI wa Leeds United, Rodrigo, mwenye umri wa miaka 32, huenda akalazimika kupunguziwa mshahara ikiwa atatia saini mkataba mpya katika klabu hiyo. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania unatarajiwa kumalizika msimu wa majira ya joto wa 2024. ***(Football Insider)***

### SAKA MSHAHARA JUU

MSHAMBULIAJI wa England, Bukayo Saka, mwenye umri wa miaka 21, atapokea takriban pauni milioni 15 kwa msimu atakapotia saini mkataba wake mpya na Arsenal. ***(Mail)***

### MILNER BADO LIVERPOOL

LIVERPOOL bado hawajaanza mazungumzo ya mkataba mpya na kiungo wa zamani wa England, James Milner, licha ya Jurgen Klopp kutaka kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, kwa mwaka mwingine. ***(Athletic)***

### CHELSEA KUUZA NYOTA

CHELSEA italazimiwa kuongeza kiasi kikubwa cha fedha kwa kuwauza wachezaji msimu huu ili kuepuka kukiuka kanuni za kifedha za Ligi Kuu England mwakani. ***(Mirror)***

### NAGELSMANN ATAKIWA SPURS

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, anataka kujua kama Julian Nagelsmann yuko tayari kuchukua nafasi ya Antonio Conte kama kocha mkuu wa Spurs. ***(Mirror)***

### NAGELSMANN AIGAWA BAYERN

KIKOSI cha Bayern Munich kimegawanyika katika makundi mawili kuhusu uamuzi wa kumfuta kazi kocha Julian Nagelsmann mwenye umri wa miaka 35. ***(Bild, via Goal)***

### FERGUSON AWINDWA SPURS

Tottenham Hotspur ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazomtaka mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 18. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# VAN PERSIE: ARSENAL ITABEBA UBINGWA EPL

●●●Wanacheza mpira mzuri sana ambao ni mzuri kutazama, wanastahili kushinda taji la ligi, ingawa itakuwa ngumu kwa sababu City...

**LONDON, England**

ROBIN van Persie ameiunga mkono Arsenal kukabiliana na tishio la Manchester City na kushinda taji la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2003-04.

'Washikabunduki' hao waliingia kwenye mapumziko ya kimataifa wakiwa na tofauti ya pointi nane dhidi ya mabingwa watetezi, vijana wa Pep Guardiola, ambao wana mchezo mkononi, na wamebakiza mechi 10 ligi kufikia ukingoni msimu huu.

Mwezi mgumu unakuja kwa Arsenal ambao ni Aprili, kwa safari za kumenyana na Liverpool na Man City pamoja na mechi ya nyumbani dhidi ya Chelsea, huku Newcastle United wakikutana nao Mei.

Arsenal wameshindwa katika harakati zao za kumaliza ukame wa taji la Ligi England na kutokuwa na uzoefu wa timu hiyo katika hali kama hizo kunazua wasiwasi, ingawa nahodha huyo wa zamani wa 'The Gunners', Van Persie, haoni kama hilo ni tatizo.

Van Persie amesema: "Arsenal wanafanya vizuri sana, wanacheza mfululizo. Wanacheza mpira mzuri sana ambao ni mzuri kutazama. Kwa maoni yangu, wanastahili kushinda taji la ligi."

"Bado itakuwa ngumu kwa sababu City itaisukuma Arsenal hadi siku ya mwisho. Ukiangalia kipindi hiki, hapa ndipo penye umuhimu wa kila pointi. Kumekuwa na michezo kadhaa migumu, lakini wamepata pointi tatu hapo."

## HABARI MICHEZO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,096,0

MECHI KALI
CHELTENHAM
VERSUS
SHEFFIELD WED
1 | 4.86
X | 3.59
2 | 1.68

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# OFA KUINUNUA MAN UNITED BADO NDOGO

**MANCHESTER, England**

ZABUNI zilizorekebishwa za kuinunua Manchester United bado hazijafikia kiwango kinachotakiwa na familia ya Glazer, ingawa bado kuna matumaini ya kuiuza, kwa mujibu wa ESPN.

Ofa za pili ziliwasilishwa na wahusika wiki iliyopita, wakiwamo Sheikh Jassim Bin Hamad Al Thani, Sir Jim Ratcliffe na Thomas Zilliacus.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba zabuni kutoka kwa Sheikh Jassim na Ratcliffe zimeongezwa kutoka takriban pauni bilioni 4.5, lakini zimesalia chini ya bei inayotakiwa ya karibu pauni bilioni sita - ingawa kuna matumaini kwamba Glazers bado wanaweza kukubali bei ya maelewano kuruhusu kuiuza klabu hiyo ya Old Trafford.

Baada ya ofa ya hivi karibuni, wazabuni wanasubiri kusikia kutoka kwa Raine Group, Benki ya Marekani inayofanya kazi na Glazers katika mchakato wa kuiuza klabu hiyo.

Wafanyakazi wa United wameambiwa kutarajia "uwazi" juu ya hali ya umiliki ifikapo mwishoni mwa msimu.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba bado ni "biashara kama kawaida," ingawa kuna kukubalika kwamba upanuzi wa mikataba kwa wachezaji muhimu - ikiwa ni pamoja na Marcus Rashford - na dirisha la uhamisho wa majira ya joto.

Wakati huo huo, wamiliki wapya wanaweza kutaka kufanya mabadiliko makubwa kwenye muundo wa klabu, ambayo inaweza kuhatarisha awamu inayofuata ya ujenzi wa kikosi chini ya kocha Erik ten Hag.

Baadhi ya vyanzo vimetaja usumbufu uliosababishwa na Todd Boehly baada ya kuinunua Chelsea, ambayo ni pamoja na kumtimua kocha Thomas Tuchel na nafasi yake kuchukuliwa na Graham Potter miezi minne tu baada ya ununuzi wake kukamilika.

Ten Hag amefanya kazi vizuri na mkurugenzi wa soka, John Murtough na timu yake tangu alipoteuliwa kuwa kocha msimu wa majira ya joto uliopita, huku Mholanzi huyo akiwa tayari ameshinda Kombe la Carabao katika msimu wake wa kwanza.



# Oxlade hajui atacheza timu gani

**LONDON, England**

ALEX Oxlade-Chamberlain anaonekana kukosa chaguo linapokuja suala la kuchagua klabu yake ijayo ikiwa ataondoka Liverpool msimu wa majira ya joto.

Chamberlain mwenye umri wa miaka 29, alijiunga na Liverpool mwaka 2017, lakini ameshindwa kuleta matokeo ya kudumu pale Anfield na mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye michezo 35 kwa taifa hilo, amekuwa sehemu ya kikosi kilichotwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu England, lakini mara chache anamaliza dakika 90 chini ya Jurgen Klopp.



Na kwa mujibu wa gazeti la The Daily Mail, Brighton, Newcastle na Aston Villa zimempanga kiungo huyo kwa ajili ya kumsajili dirisha la usajili litakapofunguliwa.

Brighton imekuwa ikihusishwa vikali na nyota huyo wa zamani wa Arsenal, lakini wakasitishwa Januari kwa mpango unaosemekana kuwa tayari kumchukua Oxlade kama mchezaji huru.

Newcastle ya Eddie Howe pia inaripotiwa kumtaka mchezaji huyo mzaliwa wa Portsmouth huku Magpies hao wakipania kuunda kikosi kitakachoweza kushinda taji hilo ndani ya miaka michache ijayo.

Lakini anaweza kuchagua kujiunga na Villa ya Unai Emery kule Midlands.

Majeraha yamemweka nje ya uwanja kwa muda mwingi wa msimu wa 2022-23.

## HABARI MICHEZO

041,286/-

# TSHABALALA NA MASTAA WA5 KUIKOSA RAJA CASABLANCA

**Na Saada Akida**

BEKI wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', ni miongoni mwa wachezaji sita wa kikosi hicho watakaukosa mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablanca utakaopigwa nchini Morocco Jumamosi wiki hii, imeelezwa.

Wachezaji hao watakaukosa mchezo huo kwa sababu mbalimbali ikiwamo kuwa majeruhi, lakini kwa Tshabalala anakosekana kutokana na kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano.

Simba jana ilianza safari kuelekea Morocco tayari kwa mchezo huo, ikiwa na wachezaji 13 tu, huku wengine wakitarajiwa kujiunga na wenzao nchini humo baada ya kukamilisha majukumu ya kuzitumikia timu zao za taifa, lakini Tshabalala hataendelea kubaki nchini kutokana na kutokuwa sehemu ya mchezo huo wa kukamilisha hatua ya makundi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji 22 ndio watakakwenda Morocco kubeba jukumu la mchezo huo na kwamba jana wametangulia 13 na waliokuwa katika timu ya Taifa ya Tanzania na mataifa mengine wataungana na wenzao nchini humo.

Alisema wanaelekea katika mchezo huo wakiwakosa baadhi ya wachezaji wao, Mohamed Ouattara, Jonas Mkude, Mohamed Mussa, Jimmyson Mwanuke na Augustine Okrah ambao ni majeruhi huku Tshabalala akikosekana kutokana na kuwa nje akitumikia kadi tatu za njano.

"Tshabalala mwenye kadi tatu za njano hatakuwa sehemu ya kikosi kitakachowavaa Raja Casablanca, siku ya Jumamosi.

"Tunatambua mchezo utakuwa mgumu na ushindani mkubwa kwa sababu Raja Casablanca mechi ya kwanza walitufunga nyumbani na wanahitaji kuweka rekodi katika uwanja wao wa nyumbani, lakini Simba tunahitaji kuweka heshima tusipoteze katika mchezo huo wa mwisho wa makundi," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa matokeo yoyote watakayopata katika mchezo huo hayataathiri msimamo wa kundi hilo kwa sababu wameshafuzu kucheza robo fainali na mechi hiyo ni ya kukamilisha ratiba tu, lakini wanataka kulinda heshima ya Simba.

Simba inakibarua katika mchezo huo dhidi ya Raja Casablanca utakaopigwa Machi 31 saa 4:00, usiku kwa Morocco na Tanzania saa 7:00 usiku, hivyo itakuwa ni Aprili Mosi, mwaka huu, katika Uwanja wa Mohammed V, nchini humo.

# Kakolanya aitesa Simba

INATOKA UK. 24

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jana kutoka ndani ya klabu hiyo, Simba wanapambana kumzuia kipa huyo kwenda kuitumikia Singida Big Stars kwa msimu ujao kwa kuhakikisha wanampa ofa anayohitaji.

Mtoa habari alidai kuwa tayari Singida Big Stars imemwingizia fedha katika akaunti yake, hivyo inachotakiwa Simba ni kukubaliana na dau ili kumpa arejeshe.

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, akizungumza na mwandishi wetu katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kabla ya kukwea pipa kuelekea Morocco kwa mchezo dhidi ya Raja Casablanca, amesema pamoja na kuwa wameshatinga hatua ya robo fainali, lakini anakwenda kupambana kwa ajili ya kusaka ushindi na kukiweka sawa kikosi chake kwa ajili ya mechi zinazofuata kwani anataka kwenda mbali zaidi ya hapo.

"Tuko kwenye kiwango kizuri sasa, kuliko mwanzo tulipokutana nao, hivi sasa wachezaji wangu wapo moto, kuna Kibu Denis, kuna kiwango bora cha Jean Baleke, halafu nyuma hapa nina Clatous Chama na Saido Ntibazonkiza.

"Wote wapo kwenye kiwango cha juu kuliko mwanzo tulipokutana nao, tunaweza kabisa kulipa kisasi, lakini tunacheza kwa ajili ya kutengeneza ufiti na kujiamini kwa wachezaji kwani timu kubwa kama ile inawafanya wachezaji wasiwe na shaka tena kucheza na timu nyingine kwenye hatua ya robo, nusu fainali na hata fainali," alisema Robertinho.

Kwa upande wa Ahmed Ally, alisema wanakwenda kucheza mechi ambayo licha ya kwamba inachezwa usiku mzito, lakini haina presha sana kwa sababu wameshatinga hatua ya robo fainali.

"Wachezaji Aishi Manula, Shomari Kapombe, Beno Kakolanya na Mdhamiru Yassin, wao wataondoka nchini Jumatano (kesho) kuja kujiunga na wenzao. Kwa wachezaji wengine ambao wapo kwenye vikosi vya timu za mataifa mengine kama Chama, Enock Inonga, Peter Banda, Pape Sakho, pamoja na Saido, wao watatoka kwenye mataifa yao kuja moja kwa moja kujiunga na kikosi.

"Kwenye kikosi hatutokuwa na Mohamed Hussein 'Tshabalala' kwa kuwa yeye ana kadi tatu za njano, pia tutawakosa baadhi ya wachezaji ambao ni majeruhi na wengine nao hawajapona vizuri, nawazungumzia Mohamed Outtara, Joans Mkude, Augustine Okra, Ismael sawadogo, Jimmyson Mwanuke na Mohamed Mussa.

"Mechi yetu itakuwa ni Jumamosi saa nne usiku kwa saa za Morocco, lakini hapa nchini ni saa saba usiku," alisema.



Raja ina pointi 13 mpaka sasa, huku Simba ikiwa na pointi tisa, hivyo matokeo ya mechi hiyo licha ya kwamba hayatoathiri timu hizo kufuzu, lakini hayatoathiri msimamo wa kundi hilo kwani hata Wekundu wa Msimbazi hao wakishinda wataishia pointi 12.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/04/23 | 17:00 | AFC Bournemouth vs Fulham FC | 2.45 | 3.10 | 2.80 |
| 02. 01/04/23 | 17:00 | Crystal Palace vs Leicester City | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 01/04/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Wolverhampton Wanderers | 2.85 | 3.00 | 2.45 |
| 04. 01/04/23 | 19:30 | Cadiz CF vs Sevilla FC | 3.05 | 3.00 | 2.33 |
| 05. 01/04/23 | 21:00 | SC Cambuur vs FC Emmen | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 01/04/23 | 22:00 | RKC Waalwijk vs Vitesse Arnhem | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 01/04/23 | 22:00 | Stade Rennes vs RC Lens | 2.36 | 3.25 | 2.80 |
| 08. 02/04/23 | 13:30 | Bologna FC vs Udinese Calcio | 2.23 | 3.15 | 3.10 |
| 09. 02/04/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Konyaspor | 2.90 | 3.50 | 2.24 |
| 10. 02/04/23 | 15:15 | Grasshopper Club Zurich vs FC Lugano | 2.47 | 3.15 | 2.41 |
| 11. 02/04/23 | 16:00 | FC Nantes vs Stade Reims | 2.90 | 3.20 | 2.33 |
| 12. 02/04/23 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Toulouse FC | 2.80 | 3.30 | 2.34 |
| 13. 02/04/23 | 16:00 | Giresunspor vs Alanyaspor | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 14. 02/04/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Boavista Porto | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 02/04/23 | 18:30 | Newcastle United vs Manchester United | 2.39 | 3.20 | 2.80 |
| 16. 02/04/23 | 18:30 | Werder Bremen vs TSG Hoffenheim | 2.23 | 3.45 | 2.85 |
| 17. 02/04/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.28 | 3.05 | 3.10 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 29/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1381 | Cheongju FC vs Seoul Jungnang FC | 1.07 | 10.38 | 14.54 |
| 13:00 | 1842 | Chungnam Asan vs Jeonbuk Maeil FC | 1.15 | 7.47 | 10.17 |
| 13:00 | 3636 | Anyang vs Busan I Park | 1.63 | 3.52 | 4.97 |
| 13:00 | 3867 | Hwaseong FC vs Ansan Greeners | 3.01 | 3.32 | 2.14 |
| 13:00 | 4142 | Seongnam Ilhwa vs Pyeongchang United | 1.36 | 4.75 | 6.40 |
| 13:00 | 4818 | Corum Bld vs Kasimpasa Erokspor | 1.97 | 3.21 | 3.57 |
| 13:00 | 5222 | Shimizu S Pulse vs Thespakusatsu | 1.53 | 3.74 | 5.33 |
| 13:00 | 5621 | Seoul E Land vs Bucheon | 2.79 | 3.04 | 2.42 |
| 13:00 | 5622 | Jubilo Iwata vs Tochigi SC | 1.89 | 3.18 | 3.75 |
| 13:00 | 5680 | Portimonense U23 vs Rio Ave U23 | 1.96 | 3.58 | 3.22 |
| 13:00 | 5821 | Jeonnam Dragons vs Mokpo City | 1.76 | 3.21 | 4.55 |
| 13:30 | 1181 | Chiangmai FC vs Rajpracha FC | 2.05 | 2.82 | 3.74 |
| 13:30 | 2419 | Bandirmaspor vs Bodrumspor | 2.24 | 3.23 | 2.82 |
| 13:30 | 3429 | Sanliurfaspor vs Duzcespor | 1.76 | 3.31 | 4.35 |
| 14:00 | 2038 | Nakhon Pathom United FC vs Ranong United | 1.38 | 3.76 | 8.44 |
| 14:00 | 2217 | Irodotos vs AEK Athens B | 3.79 | 2.91 | 2.03 |
| 14:00 | 2306 | Kocaelispor vs Duzyurtspor | 2.06 | 2.90 | 3.20 |
| 14:00 | 2580 | Serik Belediyespor vs Pazarspor | 1.56 | 3.21 | 6.84 |
| 14:00 | 3105 | Nazilli Belediye vs Inegolspor | 2.00 | 3.16 | 3.52 |
| 14:00 | 3882 | Rayong FC vs Chiangmai United | 2.00 | 3.08 | 3.49 |
| 14:00 | 4214 | Etimesgut BS vs Belediye Vanspor | 5.40 | 3.15 | 1.57 |
| 14:00 | 4543 | Kirsehir Belediye Spor vs Fethiyespor | 2.33 | 2.79 | 3.21 |
| 14:00 | 4554 | Sariyer vs Balikesirspor | 1.70 | 3.25 | 4.86 |
| 14:00 | 4590 | Sivas Dort Eylul vs Amedspor | 7.25 | 3.68 | 1.45 |
| 14:00 | 4612 | Somaspor vs Anagold 24erzincanspor | 2.42 | 3.04 | 2.79 |
| 14:00 | 5693 | Pattaya United FC vs Trat FC | 4.41 | 3.07 | 1.79 |
| 14:30 | 2265 | Phrae United vs Kasetsart University FC | 1.71 | 3.29 | 4.53 |
| 14:30 | 3078 | Uthai Thani FC vs Ayutthaya United | 2.20 | 3.03 | 3.08 |
| 15:00 | 5661 | Krabi FC vs Suphanburi | 4.11 | 2.98 | 1.88 |
| 16:00 | 2704 | Concordia Elblag vs KS Blonianka Blonie | 2.31 | 3.20 | 2.55 |
| 16:00 | 5611 | Caykur Rizespor vs Manisa BBSK | 1.87 | 3.50 | 3.45 |
| 16:30 | 1587 | Psis Semarang vs Persebaya Surabaya | 2.45 | 3.15 | 2.43 |
| 17:00 | 3553 | BDF XI vs Holy Ghost | 1.72 | 3.47 | 4.35 |
| 17:00 | 5082 | NK Fuzinar Ravne vs NK Rogaska | 3.24 | 3.49 | 1.94 |
| 17:00 | 5161 | Chelmianka Chelm vs Sokol Sieniawa | 1.84 | 3.68 | 3.53 |
| 18:00 | 2394 | SK Zapy vs Zivanice | 1.70 | 3.38 | 4.41 |
| 18:30 | 3148 | TSV Aubstadt vs Unterhaching | 3.58 | 3.47 | 1.88 |
| 18:30 | 3775 | Arman Gohar Sirjan vs Caspian Babol | 2.34 | 2.64 | 3.41 |
| 18:45 | 4927 | Chador Malu Yazd vs Saipa Karadj | 2.12 | 2.65 | 3.45 |
| 19:00 | 2087 | Khalijfars Mahshahr vs Fajr Sepasi | 2.85 | 2.75 | 2.59 |
| 19:00 | 2917 | Khosheh Talaei vs Pars Jonoubi Jam | 2.55 | 2.55 | 2.85 |
| 19:00 | 5792 | Chooka Talesh FC vs Mes Shahr-e Babak | 2.70 | 2.50 | 2.75 |
| 19:45 | 3315 | Barcelona W vs AS Roma W | 1.11 | 7.90 | 13.51 |
| 20:30 | 5819 | Egestorf/Langreder vs VfL Oldenburg | 1.56 | 3.95 | 4.10 |
| 21:00 | 2861 | Cronenberger SC vs Uerdingen | 7.68 | 5.19 | 1.29 |
| 21:45 | 1707 | Tiverton Town vs Hendon | 2.13 | 3.42 | 2.95 |
| 21:45 | 4416 | Cheltenham vs Sheffield Wed | 4.86 | 3.59 | 1.68 |
| 21:45 | 5330 | Dumbarton vs Forfar Athletic | 1.97 | 3.39 | 3.24 |
| 21:45 | 5604 | Truro City vs Bracknell Town | 2.19 | 3.51 | 2.79 |
| 22:00 | 5489 | Arsenal W vs Bayern Munich W | 1.97 | 3.57 | 3.21 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Machi 29, 2023

Nipashe




UKURASA 21

## Van Persie: Arsenal itabeba ubingwa EPL



Wachezaji wa Simba, Joash Onyango (Kushoto) na Nassoro Kapama, wakielekea Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jana, tayari kwa safari ya Morocco kwenye mechi ya kuhitimisha hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablanca itakayopigwa Jumamosi. **MPIGAPICHA WETU**

# KAKOLANYA AITESA SIMBA

●●● Singida Big Stars yachochea moto, Robertinho naye ang'aka akiifuata Raja bila Tshabalala...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU baadhi ya wachezaji wa kikosi cha Simba wakikwea pipa jana kuelekea Morocco tayari kwa mchezo wao wa kukamilisha hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablaca, Singida Big Stars inazidi kuichanganya klabu hiyo ya mtaa wa Msimbazi, Dar es Salaam kutokana na kuendelea kokamaa kuipata saini ya kipa wao namba mbili, Benno Kakolanya, imefahamika.

Simba jana iliondoka na wachezaji 13, huku ikitarajia wengine tisa kuungana nao nchini Morocco baada ya kumaliza majukumu ya timu zao za taifa.

Hata hivyo, Kakolanya ambaye anaunda kikosi cha Taifa Stars kilichokuwa na jukumu la kuivaa Uganda katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana kwenye mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, mkataba wake na Simba unamalizika mwishoni mwa msimu huu na inadaiwa kipa huyo tayari amesaini mkataba wa awali wa miaka miwili na Singida Big Stars.

Awali, ilidaiwa kuwa Simba ilikuwa tayari kumpa Sh. milioni 50 na mshahara wa Sh. milioni tano kwa mwezi ili kusaini mkataba mpya wa miaka miwili, lakini Singida Big Stars ilichungulia dili hilo na kupanda juu kwa kumwekea mezani Sh. milioni 100 na mshahara kama huo wa klabu yake kwa mwezi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa mchezaji huyo, Seleman Haroub, ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, alisema tayari mazungumzo ya awali yalifanyika na anaimani wataenda vizuri na kipa huyo kusalia ndani ya klabu hiyo.

"Ni kweli kuna baadhi ya timu zimekuwa zikimsumbua mchezaji wetu, hii ni baada ya mkataba wake kuelekea kufikia ukingoni, Mtendaji Mkuu wa Simba, Kajula (Imani) anafanya juu chini Kakolanya aendelee kusalia ndani ya kikosi cha timu yetu kwa msimu ujao," alisema meneja huyo.

Aliwatoa presha mashabiki wa Simba kuwa mteja wake huyo ataendelea kusalia ndani ya kikosi cha timu hiyo kwa sababu mazungumzo mengine yanaendelea ili kumwezesha kuendelea kuvaa jezi ya Wekundu wa Msimbazi hao kwa msimu ujao.

INAENDELEA UK. 23

## Nabi ataja wawili kuikosa Mazembe

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga kikitarajia kuifuata TP Mazembe kesho, Alhamisi kikiwa na majembe yake kamili, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Nasreddine Nabi, ametaja wachezaji wawili ambao hawatakuwa sehemu ya mpango wa mchezo huo wa kukamilisha hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga tayari imefuzu hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho na inachokitafuta kwa sasa ni kushinda na kumaliza kileleni mwa msimamo wa Kundi lao la D, wakati huu ikikalia nafasi hiyo kutokana na kuizidi US Monastir ya Tunisia kwa tofauti ya mabao tu ya kufunga na kufungwa baada ya timu hizo kila moja kuwa na pointi 10.

Katika mchezo uliochezwa Uwanja wa Mkapa ubao ulisoma Yanga 3-1 TP Mazembe, hivyo mchezo ujao utakaochezwa DR Congo Jumapili wiki hii kila timu itakuwa na kazi ya kusaka pointi, lakini hata kama miamba hiyo ya Congo itashinda bado Yanga na US Monastir itakayocheza na Real Bamako, ndizo timu zilizofuzu hatua ya robo fainali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi aliwataja wachezaji ambao hawatakuwa sehemu ya msafara wa timu hiyo kuelekea DR Congo, kuwa ni Bernard Morrison na Denis Nkane.

Alisema licha ya wachezaji hao kuanza mazoezi baada ya kupona majeraha yao yaliyowaweka nje kwa muda mrefu, hawatakuwa sehemu ya kikosi kitakachondoka Alhamisi kuelekea DR Congo katika dhidi ya wenyeji wao, TP Mazembe.

Aidha, alisema umakini na ushirikiano wa wachezaji wake utakuwa mkubwa utakaowapa nguvu kuongoza kundi lao, kwa kuwa bado hawajamaliza kazi.

Alisisitiza kuwa wachezaji wake wanapaswa kuendelea kujituma na kuongeza juhudi zaidi kuelekea katika michezo ya robo fainali kwani watakutana na timu kigogo zaidi kutoka hatua ya makundi.

"Tumefika hatua ya robo baada ya miaka mingi, ni hatua ngumu tunayokwenda kucheza, wachezaji wanatakiwa kuongeza umakini na kujituma zaidi kwa kuanza kutumia mechi dhidi ya TP Mazembe, kama sehemu ya kujiandaa na michezo ya robo na kusaka pointi tatu," alisema kocha huyo raia wa Tunisia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >